




**Mjumbe** adaiwa kutoa siri kamati ya uchunguzi NHC

UKURASA 4



**CHELSEA NJIA NYEUPE KUMNASA KOULIBALY**

UKURASA 22


# Nipashe

Alhamisi Julai 14, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581006 *

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


# Ugonjwa wa ajabu waua watu watatu

• **Ni** wa kutokwa damu puani alioutaja Rais Samia... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 13

**WAPANDA BODABODA JIFUNZENI JAMBO HILI**

MAUMIVU ya mgongo ni tatizo linalowapata watu wengi kulingana na majukumu ya kazi...

## Tume kuundwa kuchunguza vigogo kuuziwa viwanja

UKURASA 3



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe, ofisini kwake Magogoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akisikiliza maelezo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO), Prof. Frederick Kahimba (kushoto), alipotembelea banda la Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kabla ya kufunga maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam katika Uwanja wa Julius Nyerere, Barabara ya Kilwa jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



## Ajali ya gari ilivyowaua mgonjwa na wauguzaji

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA ZAKABANA KOO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Ugonjwa wa ajabu waua watatu

**Na Agusta Njoji,** DODOMA

WATU watatu kati ya 13 waliobainika kuugua ugonjwa usio wa kawaida uliozuka mkoani Lindi wamefariki dunia.

Hata hivyo, serikali imesema bado inaendelea na uchunguzi licha ya sampuli za awali zilizopimwa katika Maabara ya Taifa kuonyesha majibu hasi kwa ugonjwa wa ebola, Marburg na UVIKO-19.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo, Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, alisema Wizara ya Afya ilipokea taarifa ya kuwapo kwa ugonjwa huo katika Wilaya ya Ruangwa kwenye Kituo cha Afya Mbekenyera na ndani ya siku tatu (Julai 5 hadi 7 mwaka huu) walipokea wagonjwa wawili wakiwa na dalili za homa, kuvuja damu hususan puani, kichwa kuuma na mwili kuchoka sana.

Alisema wizara iliunda timu ya wataalamu kutoka Idara ya Magonjwa ya Dharura na Majanga, Epidemiolojia, Mkemia Mkuu wa Serikali, Taasisi ya Utafiti (NIMR), Chuo Kikuu cha Sayansi ya Tiba Muhimbili na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) ambao waliungana na timu ya mkoa ikihusisha Idara ya Mifugo.

"Hadi kufikia Julai 12, mwaka huu, kulikuwa na wagonjwa 13. Kati yao, watatu wamefariki dunia, wagonjwa wawili waliokuwa wametengwa katika Kituo cha Afya Mbekenyera, Wilaya ya Ruangwa wamepona na kurudi nyumbani, wagonjwa watano wamejitenga katika makazi yao ya muda kwenye Kitongoji cha Naungo, Kata ya Nanjilinji wilayani Kilwa," alisema.

Alibainisha kuwa kati ya wagonjwa waliopona, mmoja anaendelea kufanya shughuli zake Kijiji cha Mbekenyera.

Vilevile, alisema watu waliotangamana na wagonjwa hao wamekuwa wakifuatiliwa afya zao kila siku na hadi sasa hakuna aliyeonyesha dalili zozote zinazofanana na wagonjwa hao.

"Tunaendelea kufanya uchunguzi zaidi wa kiepidemiolojia na kitabibu, pia tunasubiri matokeo ya vipimo zaidi vya maabara ya magonjwa ya binadamu, wanyama na Mkemia Mkuu wa Serikali," alisema.

Alitaja hatua zingine zinazoendelea kuchukuliwa na wizara hiyo kuwa ni kutafuta watu wengine wenye dalili hizo ili kutambua mapema na kuwatenga ili kuzuia ugonjwa usisambae.

"Kuorodhesha watu wote waliotangamana na wagonjwa au marehemu na kuwafuatilia kwa siku 21, kutoa matibabu kwa wagonjwa waliobainika kuwa na dalili pia kuwashauri wajitenge wakati wakisubiria majibu ya vipimo vya maabara, kutoa elimu kwa jamii kwa kutumia vyombo mbalimbali vya habari," alisema.

Pia alisema yamefanyika maandalizi ya dawa, vifaa tiba na vifaa vya kujikinga na maambukizi kwa ajili ya kuwahudumia waathirika endapo watajitokeza tena.

Alitoa wito kwa wananchi kuwa watulivu wakati serikali ikiendelea kulifanyia kazi suala hilo na kuwasisitiza kutumia vituo vya kutolea huduma za afya watakapojisikia kuumwa.

Kuwapo kwa watu wanaougua ugonjwa huo nchini, kuliwekwa bayana juzi na Rais Samia Suluhu Hassan, alipohutubia mkutano wa 20 wa Shirikisho la Baraza la Maaskofu Katoliki Afrika Mashariki na Kati (AMECEA) jijini Dar es Salaam.

Rais Samia alisema: "Kuna kila aina ya maradhi mapya yanazuka ambayo hatujayui. Nilikuwa ninazungumza na Waziri Mkuu, juzi alitoka kwenye ziara kusini, Lindi, ananiambia ameona kuna maradhi yameingia wanadamu wanatokwa tu damu za pua na wanadondoka.

"Hatujui ni kitu gani, wanayasansi, wataalamu wa afya wote wamehamia huko wanaangalia ni kitu gani. Kwanini mwanadamu atokwe tu na damu kwenye pua, adondoke? Angekuwa mmoja, wawili tungesema presha imepanda lakini ni wengi kwa mfululizo," alibainisha.




Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo (wa pili kushoto), akishirikiana na Naibu Katibu Mkuu CCM Bara, Christina Mndeme (kushoto), pamoja Katibu wa CCM mkoa wa Dodoma, Pili Mbanga (kulia), wakifungua pazia kuweka jiwe la msingi la eneo la biashara la chama hicho, kwenye Uwanja wa Barafu, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ajali ya gari ilivyowaua mgonjwa na wauguzaji

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WATU watatu wa familia moja, akiwamo mtoto mdogo, wakazi wa Kata ya Terati katika Halmashauri ya Jiji la Arusha, wamepoteza maisha kwa ajali baada ya kugongwa na gari wakati wanatoka hospitalini wakiwa wamepakizana kwenye pikipiki.

Tukio hilo lilitokea majira ya saa 10.45 usiku wa kuamkia jana katika barabara ya mchepuo ya Arusha wakati watatu hao walipokuwa wanatoka hospitalini kumpeleka mtoto Ebenezer Mollel mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu aliyekuwa ameandikiwa sindano za saa.

Wengine waliofariki dunia ni mama wa mtoto, Neema Mollel (27) na mdogo wake, Agustino Mollel (24) ambaye alikuwa dereva wa pikipiki.

Kwa mujibu wa shuhuda wa tukio hilo, John Mushi, watatu hao walipoteza maisha eneo la tukio baada ya kupata majeraha makubwa na kuvuja damu nyingi. Alisema walishuhudia miili ya marehemu hao ikiwa na mivunjiko mingi na kusagika mikono na miguu huku mtoto na dereva wakipasuka kichwa.

Kaka wa Neema na Augustino, Daud Mollel, alisema ndugu zake waligongwa kwa nyuma wakiwa wamepakizana kwenye pikipiki na gari ambalo halikujulikana kutokana na kusababisha ajali.

Alisema kuwa baada ya kupata taarifa juu ya ajali hiyo, alifika eneo la tukio na kushuhudia miili ya marehemu ikiwa na majeraha makubwa sehemu mbalimbali za miili yao.

"Walitoka nyumbani Terati majira ya saa 10 usiku kwenda Hospitali ya Murieti, baada ya mtoto (marehemu) kuandikiwa sindano za saa, wakati wakirudi majira ya saa 10:45 usiku ndipo walipogongwa na gari kwa nyuma na kufariki dunia,"alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, alithibitisha tukio hilo na kubainisha kuwa walikuwa kwenye uchunguzi zaidi.

Kamanda Masejo alisema gari lililohusika na tukio hilo halikupatikana na polisi wanaendelea na uchunguzi ili kumtia mbaroni dereva wa gari hilo aliyetoweka baada ya ajali hiyo.

Miili ya watatu hao imehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhi maiti kwenye Kituo cha Afya Murieti kwa ajili ya utaratibu wa uchunguzi.

# Chongolo abaini mchezo mchafu kuelekea 2025

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKATI joto la uchaguzi wa ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) likiendelea kupanda, Katibu Mkuu wa Chama hicho, Daniel Chongolo, amebaini kuwapo mchezo mchafu unaofanywa na baadhi ya watu wanaopanga safu za uongozi mwaka 2025.

Kutokana na hali hiyo, ametoa onyo kwamba wanaojihusisha na mchezo huo watashughulikiwa kwa viwango vinavyostahili huku akiagiza vikao vitakavyotumika kuchuja wagombea kutoona aibu kuwachukulia hatua watakaokiuka kanuni.

Akifungua jana mafunzo ya uongozi kwa viongozi wa mashina na matawi wa chama hicho waliochaguliwa hivi karibuni mkoani Dodoma, Chongolo alisema wakati uchaguzi ndani ya chama unaendelea, kuna mambo yanafanyika ambayo yanakiuka Katiba ya chama na kanuni ikiwamo rushwa na kupanga safu za uongozi za ubunge na udiwani kwa ajili ya mwaka 2025.

"Kubwa ambalo linasikitisha zaidi ni baadhi ya watu wenye ndoto ya nafasi zingine mpaka sasa, wabunge wote nchi nzima hao ni wabunge wamepewa dhamana na chama hichi na mimi kazi yangu ni kuwalinda hadi 2025. Yeyote mwenye lengo la nafasi hiyo asubiri hadi 2025. Usijipime leo kwa kupanga watu wa kukufanyia mambo yako mbeleni.

"Kuna watu wako 'busy' wanapita huko kazi wanayofanya ni kutafuta wapange watu watakaoingia kwenye nafasi ili kuwasaidia kwenye malengo yao ya baadaye. Niwaambie tunawaona, tunawajua na mnayofanya tunayajua na mimi ni kijana nawapa pole mnaofikiria 2025 sitakuwa na fursa na nitakuwa siyajui mnayoyafanya, tuta 'deal' nao kwa kiwango kinachowastahili," amesema.

"Ahadi ya nne ya mwana CCM inasema rushwa ni adui wa haki sitatoa wala kupokea rushwa. Naomba sana zifanyike kampeni bila hila, kusingiziana, kutengenezeana uzushi na uongo. Kila mmoja atumie yale mema ambayo anaamini ana uwezo nayo na si kutumia uongo na uzushi kwa kuwa baada ya uchaguzi tutatengenezeana nongwa zisizo na msingi," alisisitiza.

Alisema anayefikiri ana dhamana ya kutofuata maagizo na maelekezo ya chama atakuwa amelazimisha kuchukuliwa hatua na chama hakitasita kuchukua hatua kwa kuwa hakioni faida wala hasara ya kulea watu wanaokiuka taratibu.

Chongolo alisema wanachama bado wanajitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi huku akisema upo mkoa mmoja hadi sasa wanachama 100 wamejitokeza

HABARI KITAIFA

# Tume kuundwa uchunguzi vigogo kuuziwa eneo nyeti

**Na Richard Makore,**
MWANZA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Anjelina Mabula, ameagiza kufanyika uchunguzi wa kina kuhusu eneo la Isamilo ambalo linadaiwa kuuzwa kwa vigogo wa serikali ili kubaini kama njia walizotumia kupata viwanja hivyo, zilifuata utaratibu.

Eneo hilo lenye viwanja 39, linalalamikiwa na wananchi kuwa lilichukuliwa bila wao kulipwa fidia na kuuzwa kwa vigogo hao wa serikali.

Dk. Mabula pia amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi, kuunda tume huru ambayo itafanya uchunguzi wa kina kuhusu viwanja hivyo.

Alitoa agizo hilo jana jijini Mwanza alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu wizara yake ikiwamo mipango ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2022/23.

Alikiri kwamba eneo hilo la Isamilo ambalo lipo katikati ya Jiji la Mwanza, viwanja vyake vimeuzwa kwa vigogo hao, akitaka tume hiyo ifanye uchunguzi wa kina na kumpatia majibu ya nini cha kufanya.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa hivi karibuni katika tovuti ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza na vigogo hao ni pamoja na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Alphayo Kidata, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja.

Wengine waliouziwa viwanja hivyo ni pamoja na Mbunge wa Nyamagana, Stanslaus Mabula, Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza, Sekiete Yahaya, Meya wa Jiji hilo, Sima Costantine Sima, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Ngusa Samike, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Amon Mpanju, na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, ambaye alipata sehemu nyingine ya Luchelele.

Wengine ni pamoja na mtoto wa Magufuli, Michael Magufuli pamoja na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Said Meck Sadick.

Dk. Mabula alisema licha ya kuwa kila mtu wakiwamo watumishi wa umma wana haki ya kununua viwanja vinavyouzwa na serikali, lazima wawe wamefuata utaratibu.

Jiji hilo la Mwanza lilitangaza kuuza viwanja hivyo katika maeneo ya Isamilo na Luchelele kuanzia Juni 2, mwaka huu na kila mwombaji alitakiwa kulipia Sh. 20,000 kwa ajili ya kuchukua fomu.

Fedha hizo zilikusanywa na Jiji la Mwanza huku wananchi wa kawaida wakijitokeza kulipia ili waweze kupata viwanja vya makazi na biashara.

Kwa mujibu wa tangazo hilo la kuwapatia viwanja, wanatakiwa kufika ofisi za jiji kuchukua ankra ya malipo ili wakavilipie.

Mmoja wa wananchi waliomba kununua viwanja hivyo ambaye hakutaka jina lake liandikwe, alisema alilipia benki Sh. 20,000 kwa ajili ya kuomba kiwanja eneo la Luchelele, lakini hakuwahi kujulishwa kama alipata ama alikosa.

Alisema tangazo lililotolewa kwa wananchi wakati wa kutangaza kuuza viwanja hivyo, lilisema eneo



la Luchelele mita moja ya mraba ilikuwa ikiuzwa Sh. 5,000 kwa viwanja vya makazi.

Aliongeza kuwa eneo la Isamilo mita moja ya mraba ilikuwa ikiuzwa Sh. 25,000 ambavyo vilikuwa vichache katika mradi huo.

Katika maeneo hayo mawili, tangazo hilo pia lilisema kulikuwa na viwanja kwa ajili ya makazi na biashara.

Tangazo la Jiji la Mwanza lilisema watu waliopatiwa viwanja hivyo, walitakiwa kwenda kuchukua ankara za malipo kuanzia Juni 23 hadi Juni 30 mwaka huu.

Katika eneo la Luchelele, watu 427 wametangazwa kupatiwa viwanja hivyo huku viwanja vilivyotangazwa Isamilo vikiwa ni 39 ambavyo vimechukuliwa na vigogo.

Wiki iliyopita alipoulizwa kuhusu vigogo hao kupatiwa viwanja, Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza, Sekiete Yahaya ambaye ameuziwa kiwanja eneo hilo la Isamilo, alimtaka mwandishi kwenda ofisini kwake na wananchi wanaolalamika.

Akizungumzia kuhusu migogoro ya ardhi inayoendelea katika maeneo mbalimbali nchini, Dk. Mabula alisema moja ya vipaumbele vya wizara yake ni kuhakikisha inamaliza migogoro yote kwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan hataki kusikia suala hilo.

Alisema moja ya mipango ya kukabiliana na suala hilo ni pamoja na kuimarisha tume za mipango za ardhi ngazi ya mikoa pamoja na kuimarisha mabaraza ya ardhi ngazi za wilaya zote nchini.


twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

## UNAUDITED RESULTS
FOR THE SIX MONTHS ENDED 30 JUNE 2022

**CHAIRMAN'S STATEMENT**
Tanzania Portland Cement Public Limited Company (TPCPLC) continues to deliver strong operating results when compared to the same period 2021. Both the sales volume and revenue increased compared to the same period 2021. Revenue increased by 7.9% compared to the same period last year. This increase is due to the increased demand of cement products within Tanzania and outside Tanzania, notably in the infrastructural projects.

The improved operating performance and the availabilty of the plant and machinery attributed to the improved performance compared to the same period 2021, all within an environment where the Health and Safety of our employees and contractors is paramount. The Company continues to focus on delivering excellent customer service, selling of high quality products and maintaining strong customer relationships to enable TPCPLC to demonstrate its strength as the leading player in the industry.

| INCOME STATEMENT | JAN - JUN 2022 TZS'000 | JAN - JUN 2021 TZS'000 |
|---|---|---|
| Revenue | 227,512,642 | 210,825,663 |
| Cost of sales | (139,272,410) | (126,277,122) |
| **Gross profit** | **88,240,232** | **84,548,541** |
| Other operating income | 212,412 | 821,403 |
| Selling and administrative expenses | (1,413,469) | (1,552,643) |
| Administrative expenses | (10,468,251) | (9,314,386) |
| Depreciation and amortisation | (10,442,081) | (8,681,096) |
| Other operating expenses | (958,201) | (1,091,706) |
| **Operating profit** | **65,170,642** | **64,730,113** |
| Financial items | 2,131,055 | 1,298,145 |
| **Profit before tax** | **67,301,697** | **66,028,258** |
| Taxes on income | (20,248,978) | (19,937,458) |
| **Profit for the year** | **47,052,719** | **46,090,800** |

| BALANCE SHEET | 2022 TZS'000 | 2021 TZS'000 |
|---|---|---|
| ASSETS | | |
| Intangible fixed assets | 909,928 | 797,216 |
| Tangible fixed assets | 141,397,837 | 130,771,416 |
| Other non-current assets | 7,232,854 | 4,286,500 |
| **Non.current assets** | **149,540,619** | **135,855,132** |
| Inventories | 86,107,493 | 69,747,539 |
| Trade and other receivables | 70,387,157 | 60,811,816 |
| Cash and cash equivalents | 58,774,862 | 73,260,020 |
| **Current assets** | **215,269,512** | **203,819.375** |
| **TOTAL ASSETS** | **364,810,131** | **339,674,507** |
| EQUITY & LIABILITIES | | |
| **Equity** | **249,118,402** | **230,868,930** |
| Lease liabilities | 6,145,443 | 3,196,726 |
| Long term provisions | 9,324,932 | 6,621,779 |
| Provision for deferred taxes | 10,435,603 | 12,940,597 |
| **Non-current liabilities** | **25,905,978** | **22,759,102** |
| Lease liabilities | - | - |
| Current income tax payable | 769,868 | 3,447,885 |
| Trade and other payables | 86,247,190 | 79,801,715 |
| Dividend payable | 2,768,693 | 2,796,875 |
| **Current liabilities** | **89,785,751** | **86,046,475** |
| TOTAL EQUITY & LIABILITIES | 364,810,131 | 339,674,507 |

**Prospects**
The cement demand in Tanzania and in the East-African region has been growing steadily in recent years. TPCPLC is well placed to meet this growing demand and will continue to work to maintain its leadership. However, the on-going world crisis is putting pressure on operating margins given rising costs and posing logistical challenges for lead times of critical materials and spares.

**Appreciation**
The Board would like to thank all its stakeholders for their support. We have every confidence that TPCPLC will continue to deliver value for the shareholders and community in the future.

BY ORDER OF THE BOARD

Hakan Gurdal
Chairman of the Board
12.07.2022

Tanzania Portland Cement Public Limited Company
P.O.Box 1950
Dar-es-salaam
Tanzania
www.twigacement.co.tz
Email: info@twigacement.co.tz

216942002




Mkuu wa Biashara ya Kadi Benki ya NMB, Philbert Casmir (katikati), akimwonyesha Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Dk. Amina Ameir Issa, jinsi ya matumizi ya mashine ya kupokea malipo kwa ajili ya wizara hiyo, mjini Zanzibar jana. NMB imekabidhi mashine 50 ambazo zitasaidia kuimarisha na kukuza ukusanyaji wa mapato kwenye sekta ya utalii. Kushoto ni Meneja Biashara NMB Zanzibar, Naima Said Shaame. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mjumbe adaiwa kutoa siri za kamati ya uchunguzi NHC

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Citizen, Thomas Mosoba, amedai kuwa mmoja wa wajumbe katika kamati iliyoundwa kumchunguza Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Nehemiah Mchechu, alitoa taarifa za madai ya ubadhirifu kuhusu kiongozi huyo.

Mosoba alitoa madai hayo juzi katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam wakati akitoa ushahidi wa utetezi katika kesi iliyofunguliwa na Mchechu kwa madai ya kuchafuliwa na gazeti hilo. Gazeti la The Citizen toleo la Machi 23, 2018 lilichapisha habari yenye kichwa 'Why JPM dissolved NHC Board, sacked Mchechu', kwa tafsiri isiyo rasmi 'Kwa nini JPM (John Magufuli - aliyekuwa Rais) alivunja Bodi ya NHC, kumfukuza Mchechu'.

Kutokana na madai hayo, Mchechu ambaye aliondolewa katika nafasi hiyo kabla ya kurejeshwa miezi michache iliyopita na Rais Samia Suluhu Hassan, amefungua kesi ya madai akitaka gazeti hilo kumlipa Sh. bilioni tatu.

Akihojiwa na Jaji Leila Mgonya anayesikiliza kesi hiyo, bila kumtaja mjumbe huyo, Mosoba alidai kuwa kutokana na kupewa taarifa na mtu wa ndani ya kamati, waliamini kuwa ni taarifa sahihi, hivyo wakaamua kuzichapisha.

Alipoulizwa kama aliiona ripoti ya kamati pamoja na mapendekezo yaliyotolewa, alijibu kwamba hakuiona bali kutokana na kumwamini mjumbe pamoja na kwamba suala hilo lilikuwa mwendelezo wa aliyoyazungumza Rais John Magufuli Desemba, 2017 waliamini ni kweli.

Wakili wa Mchechu, Aliko Mwamanenge, awali alimhoji shahidi huyo kama hakukuwa na umuhimu wa kumtafuta mlalamikaji na kudai kuwa hakukuwa na ulazima kutokana na kumwamini mtoa taarifa wao.

Katika ushahidi wake, Mosoba aliwasilisha ushahidi wa video kutoka taarifa ya habari ya runinga ya Azam na Moa Online TV kuonyesha kwamba pia ni chanzo cha habari kuwa JPM alimfukuza Mchechu na kuivunja Bodi ya NHC.

Baada ya video hizo kuonyeshwa mahakamani, Wakili Mwamanenge alimhoji ni sehemu gani inayothibitisha madai hayo kuwa mteja wake alifukuzwa kazi na Rais kama ilivyodaiwa, huku akisisitiza kuwa ndio ukweli kuhusu habari hiyo.

Jaji aliruhusu video hizo zionyeshwe kwa mare nyingine lakini hakuna sehemu iliyoonyesha kuwa JPM alitamka kuwa amemfukuza Mchechu.

Mwamanenge pia alimhoji shahidi kuhusu neno 'sacked' kama lilivyoandikwa katika habari hiyo na kueleza kuwa hawakuwa na maana ya kufukuzwa bali kuondolewa katika nafasi aliyokuwa nayo Mchechu.

Kutokana na majibu hayo, Mwamanenge alichukua Kamusi ya Oxford ya Kiingereza- Kiswahili na kusoma kuwa maana ya 'sack' kwa Kiswahili ni kufukuzwa kazi, kumfukuza mtu kazi au kufukuzwa kazini. Alitoa tafsiri hiyo akijenga hoja kuwa gazeti hilo lililenga kuuhabarisha umma kwamba Magufuli alimfukuza kazi Mchechu.

Kuhusu haki ya mtu kusikilizwa kama ilivyobainishwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) juu ya maadili ya wanahabari, shahidi huyo alidai kuwa hawafungamani nayo kwa kuwa hayako kisheria bali wanafuata Sera ya Uhariri ya Nations Media Group inayomiliki kampuni ya Mwananchi Communications Limited, inayochapisha gazeti la The Citizen.

Alipohojiwa kama katika sera hiyo inatoa nafasi ya mtu kupewa nafasi ili kupata mizania ya taarifa inayomhusu, alijibu kuwa ipo na inasisitiza kuwa mtu anapaswa kupewa nafasi ya kusikilizwa.

**CHANZO CHA MADAI**

Katika habari hiyo iliyobeba uzito wa juu, ilidaiwa kuwa Mchechu alikuwa akichunguzwa na vyombo mbalimbali ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuhusu mgongano wa kimaslahi juu ya utafutaji na upatikanaji wa ekari 500 za mradi wa NHC wa Safari City jijini Arusha.

Ilidaiwa kuwa ardhi hiyo awali iliripotiwa kununuliwa na kampuni inayomilikiwa na Mchechu kutoka kwa raia wa kigeni na kuiuza NHC kwa bei ya juu.

Pia kwa mujibu wa habari hiyo, Mchechu alidaiwa kumtumia mkandarasi wa NHC kutengeneza barabara kwenda kwenye eneo lake lililo karibu na mradi wa Safari City kwa gharama za shirika.

Taarifa hiyo pia ilidai kwamba kampuni ya PHILS International ya Dubai ilipewa kazi katika mradi wa Kawe kwa uamuzi wa Mchechu bila kumhusisha Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi cha NHC, Hamisi Mpinda.

Habari hiyo pia ilidai kuwa uchunguzi ulikuwa ukifanywa kuhusu madai ya kampuni ambayo mke wa Mchechu ni mkurugenzi kupewa mkataba wa huduma ya bima kwa ajili ya nyumba za NHC mkoani Mtwara, jambo ambalo ni kinyume cha kanuni za utumishi wa umma juu ya mgongano wa kimaslahi.

Aidha, kwa mujibu wa habari hiyo, vyanzo vya habari vilibainisha kwamba kiamati iliyoundwa kuchunguza matumizi mabaya ya ofisi ndani ya NHC ilionyesha ukiukwaji mkubwa na matumizi mabaya ya kutisha ya fedha za umma uliofanywa na Mchechu.

Kutokana na habari hiyo, Mchechu alidai kuwa imemshushia hadhi, kukosa kuaminika na kupoteza nafasi nyingi za kibiashara alizokuwa akifanya pamoja na kukimbiwa na wabia katika kampuni ambazo ana uhusiano nazo.

Pia alidai kuwa kutokana na taarifa hiyo, alipata mfadhaiko, msongo wa mawazo na kuonekana ni tapeli, mlafi, mtu anayetumia vibaya nafasi yake na hata kukosa uaminifu katika kanisa ambalo ni mtumishi kwa nafasi ya uzee wa kanisa.

# Auawa na polisi akidaiwa jambazi

**Restuta Damian,** BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera limemuua kijana anayekadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka 30 na 35 baada kudaiwa kuvamia na kupora Sh. milioni 19.7 katika duka la mfanyabiashara Mussa Maduhu (38), mkazi wa Kata ya Nemba wilayani Biharamulo mkoani Kagera.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana, Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, William Mwampaghale, alisema kuwa juzi majira ya 1:45 usiku huko katika Kijiji cha Nemba, Kata ya Nemba wilayani Biharamulo, majambazi wanne walivamia dukani na kulipua baruti.

Kamanda huyo alisema majambazi hao walipofika kwenye duka la mfanyabiashara huyo, walilipua baruti na kumtisha mlinzi na kukimbia akihofia usalama wake.

"Mlinzi alikimbia kwa kuhofia usalama wake na majambazi kuanza kuvunja duka hilo na kupora fedha pamoja na vocha za mitandao ya simu ya Airtel na Tigo ambazo bado hazijafahamika thamani yake," alisema.

Kamanda Mwampaghale alisema ili kufanikisha kukamata majambazi hao, waliweka mitego katika Kijiji cha Mgera, Kata ya Nyakanazi na kufanikiwa kuwaona wakiwa na pikipiki yenye namba za usajili MC 489 DJH aina ya King lion.

Alisema askari waliokuwa wakifuatilia tukio hilo waliwasimamisha lakini walikataa kusimama, ndipo walipiga risasi hewani na wao kuanza kulipua baruti.

"Askari walipoona wamekaidi walifyatua risasi na kuwajeruhi watu wawili, mmoja ambaye hajafahamika jina alifariki dunia akiwa njiani kupelekwa hospitalini, lakini wengine walikimbia," alisema.

Aliongeza kuwa majambazi hao walikuwa na silaha za jadi zikijumuisha shoka na mtambo wa kulipua baruti ambazo waliziteleza baada ya kuzidiwa.

**HABARI KITAIFA**

# Waziri aiweka mtegoni halmashauri kuhusu mashamba yasiyoendelezwa

**Na Munir Shemweta,** SERENGETI

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameipa wiki mbili halmashauri ya wilaya ya Serengeti mkoani Mara kumpatia taarifa ya hali ya mashamba 36 ili yale yasiyoendelezwa yabatilishwe umiliki wake.

Hatua hiyo inatokana na taarifa ya sekta ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti kuwa kuna mashamba 36 yaliyopimwa na wakati wizarani hakuna kumbukumbu za kutosha kuhusu mashamba hayo.

Taarifa hiyo iliyosomwa na Ofisa Ardhi Mteule wa Halmashauri, Orwaka Nyamsusa, ilieleza kuwa mashamba hayo yalipimwa vijijini bila kufuata taratibu za uhaulishaji na ilipotakiwa yamilikishwe kwa kupewa hati za kawaida ilishindikana.

"Ninawapa Serengeti wiki mbili nijue status (hali halisi) ya mashamba hayo na kama ni suala la kuanza kuyabatilisha, mchakato uanzie katika halmashauri ambayo ni mamlaka ya upangaji ili tuitangaze fursa kwa wawekezaji kama Serengeti tunayo mashamba 36 na kati ya hayo ni matano tu yenye umiliki halali," alisema.

Akizungumza na uongozi wa wilaya ya Serengeti na watendaji wa sekta ya ardhi juzi, Dk. Mabula alisema haiingii akilini mashamba pamoja na ardhi kuwa katika halmashauri lakini halmashauri husika haina kumbukumbu iwapo imeyapima na badala yake inakwenda kutafuta kumbukumbu wizarani. Alibainisha kuwa kama utaratibu wa kuisimamia sekta ya ardhi kwa halmashauri utakuwa ni wa aina hiyo, basi haiwezi kufika popote katika masuala ya ardhi.

Halmashauri ni mamlaka za upangaji kwa mujibu wa Sheria Na. 8 ya Mipango Miji ya 2007. Ni mamlaka za upangaji zinazotakiwa kupanga miji yao wanataka iwe ya namna gani na wizara kazi yake ni kusimamia na kuangalia kama shughuli za ardhi zinaenda kwa utaratibu au sheria zinafuatwa," alisema.

Mabula alisema halmashauri nyingi hazifuati takwa la sheria huku zikifahamu ni mamlaka za upangaji na kueleza kuwa halmashauri zote zinatakiwa kutekeleza takwa hilo na zisipotekeleza migogoro ya ardhi haiwezi kuisha.

Katika taarifa yake, Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti ilieleza kuwa wilaya hiyo ina vijiji 78 na kati ya hivyo, 61 vimepimwa huku 10 vikitakiwa kufanyiwa marejeo kutokana na makosa katika ramani za upimaji.

Pia vijiji 29 kati ya 78 vina mpango wa matumizi bora ya ardhi na katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23 halmashauri hiyo imetenga Sh. milioni 15 kwa ajili ya mpango wa matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji 3.

## Mbaroni tuhuma kumuua mkewe

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linawashikilia watu wawili akiwamo Omary Lucas (48) kwa tuhuma za kumuua mke wake, Elizabeth Lusana (61), kwa kumkata kwa kitu chenye ncha kali.

Pia linamshikilia, Amos Lucas (29), kwa tuhuma za kumficha mtuhumiwa huyo ambaye ni kaka yake.

Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Ramadhan Ng'anzi, alithibitisha jana kuwashikilia wawili hao na kusema kuwa tukio la mauaji lilitokea Julai 11 mwaka huu katika maeneo ya Mtaa wa Kagera, Kata ya Lwahima wilayani Nyamagana.

"Mtuhumiwa Omari Lukas mnamo Julai 11 majira ya saa saba usiku, alimjeruhi Elizabeth kwa kumkata na kitu chenye ncha kali maeneo mbalimbali ya mwili hatua iliyosababisha kupoteza maisha.

"Uchunguzi wa awali umebaini kuwa wanandoa walikuwa na ugomvi uliotokana na wivu wa mapenzi kwa kuwa mwanaume alikuwa akimtuhumu mke wake kuwa na uhusiano usiofaa nje ya ndoa uliosababisha mauaji hayo," alisema.

Kamanda Ramadhan alisema mtuhumiwa baada ya kutekeleza tukio hilo, alitoroka na kwenda kujificha mkoani Tabora kwa Lucas ambaye naye anashikiliwa na jeshi hilo kwa kumficha mtuhumiwa.

Katika hatua nyingine, Jeshi la Polisi limethibitisha kutokea kifo cha mtoto Ally Sipendeki (5) aliyeungua katika ajali ya moto iliyotokea katika nyumba aliyokuwa akiishi na wazazi wake maeneo ya Nyabulogoya, chanzo kikiwa ni shoti ya umeme.




Mwenyekiti ya Bodi ya Wadhamini ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Jenerali mstaafu George Waitara (kulia), akisalimiana na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Daniel Sillo, baada ya kuwasili katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waonya matumizi holela sare za Jeshi

**Na Jenifer Gilla**

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA) limekemea kitendo cha baadhi ya watu kutumia sare za Jeshi la Uhifadhi Wanyamapori na Misitu kwa shughuli zao binafsi kwa kuwa ni kinyume cha sheria za jeshi hilo.

Taarifa iliyotolewa jana na Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Mawasiliano wa TANAPA, Pascal Shelutete, ilibainisha kuwa hivi karibuni yamejitokeza matukio ya uvaaji holela wa sare za jeshi hilo na kuwa kufanya hivyo, ni kinyume cha sheria.

"Hali hii imejitokeza pengine kwa kujua au kutokujua kuwa kufanya hivyo ni kinyume cha sheria iliyoundwa na Jeshi la Uhifadhi Wanyamapori na Misitu kupitia Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori na Misitu Na. 5 mwaka 2009, pamoja na marekebisho yake kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 ya Mwaka 2020," Shelutete alibainisha katika taarifa yake hiyo. Aliwataka Watanzania kuacha kutumia sare hizo mahali popote na kuwa jeshi hilo halitosita kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wote watakaobainika kukiuka maagizo hayo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua madhubuti zichukuliwe kudhibiti ajali za barabarani

**NDANI** ya saa 24, nguvu kazi ya watu 13 wamefariki dunia kwa sababu ya ajali za barabarani ambazo zimetokea katika eneo la Busiri, barabara kuu ya Lusahunga, Biharamulo mkoani Kagera na nyingine nje kidogo ya mji wa Bariadi, mkoani Simiyu huku majeruhi wakiwa 11.

Ajali ya kwanza wamefariki dunia watu wanane akiwamo mama na watoto wake wanne waliokuwa wanasafiri kwenda Ngara. Chanzo cha ajali hiyo kimeelezwa kuwa ni uzembe wa dereva wa lori lililokuwa linatokea Rwanda na katika ajali ya pili chanzo ni mwendo kasi wa dereva wa gari mojawapo.

Matukio ya ajali kwa sasa yameongezeka na kumekuwa na taarifa juu ya matukio hayo siku hadi siku. Mfano, Juni 5, mwaka huu, watu watano walipoteza maisha na wengine kujeruhiwa katika ajali iliyotokea eneo la Inyala, mkoani Mbeya, chanzo kikiwa lori lililobeba shehena ya mahindi kufeli breki na kugongana na basi dogo.

Ajali nyingine ni ya treni iliyotokea Kata ya Malolo mkoani Tabora na kusababisha vifo vya watu wanne na 132 kujeruhiwa.

Kama vile haitoshi, Juni 25, mwaka huu, watu sita wakiwamo wanne wa familia moja katika eneo la Inala, mkoani Tabora, wakati wakienda kwenye mazishi ya mama yao, walifariki dunia chanzo kikidaiwa ni gari hilo kuhama upande wake na kwenda kwenye uvungu wa lori.

Julai 9, mwaka huu, askari wawili wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) wa kikosi cha 825 KJ kambi ya Mtabila wilayani Kasulu, Kigoma, walifariki dunia na wengine wanne kujeruhiwa baada ya gari walilokuwa wakisafiria kuacha njia na kupinduka.

Wimbi la ajali limeendelea kurindima baada ya jana wanafamilia watatu kufariki dunia katika ajali wakati wakitoka hospitalini kumpeleka mtoto wa mwaka mmoja na nusu kupata sindano za saa.

Pikipiki yao iligongwa kwa nyuma na kisha kukanyangwa na gari na miili yao kuharibika.

Kutokana na ajali hizo, watu 87 wamefariki dunia kuanzia Juni 5, mwaka huu. Hizo ni ajali chache kati ya nyingi zilizoripotiwa huku kukiwa na za watu kugongwa na magari, bodaboda na bajaji.

Kwa hali ilivyo, ni lazima sasa taifa sasa kuona hili ni tatizo kubwa linalomeza watu wetu, kusababisha ongezeko la umaskini, mzigo kwa familia kutunza na kuuguza majeruhi, kuongeza wenye ulemavu ambao ni tegemezi wanaoshindwa kuhudumia familia zao ambazo nazo zinakuwa tegemezi.

Ajali hizo pia zinasababisha hospitali kuelemewa na majeruhi pamoja na familia kubeba mzigo mkubwa wa gharama.

Kasi ya madereva kutoheshimu kwa hiari sheria za usalama barabarani inaongezeka na ndiyo maana siku hizi ajali ni tukio linaloongoza kuteketeza maisha ya wananchi.

Kwa ujumla, kampeni za kukabiliana na ajali hizi zinapaswa kufanyika huku viongozi wa kila ngazi wakiwakumbusha madereva kuwa makini wanapokuwa barabarani. Kinyume cha hapo, tatizo hilo litaendelea huku taifa likizidi kupoteza mamilioni ya kodi.

Pia nguvu kazi na umaskini vitaingia kwenye baadhi ya familia hasa ambazo baba au mama aliyekuwa anategemewa kwa kila kitu anapofariki dunia au kujeruhiwa na kuuguzwa kwa muda mrefu na hatimaye kupata ulemavu wa kudumu ambao utasababisha ashindwe kufanya shughuli za kuingiza kipato katika familia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tusomeshe wanawake, ndiyo wenzetu walioshika usukani

Na Adam Fungamwango

**NIMESIKIA** kuwa baadhi ya wanawake huko Songwe wanadaiwa kuwa vinara wa kuwashawishi mabinti zao wasifanye vizuri kwenye mitihani ya shule, ili wasifaulu. Lengo kubwa hapo ni kwamba waozeshwe .

Sababu kubwa inayotawala hapo ni tamaa ya kujipatia mali. Hilo limetamkwa na Diwani wa Viti Maalum wa Kata ya Garula, Pascalina Shitundu, akiwatuhumu wanawake wenzake kwenye kijiji cha Ilasilo.

Diwani huyo 'akawapasha' wanawake wenzake kwenye mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Shirika la Maendeleo la ADP, linalohusika na masuala ya chakula cha familia.

Mwanasiasa huyo 'akawapasha' kinamama wenzake, akiwapa 'vipande' vyao kwamba wanakiuka haki za msingi wa watoto, kwa kuchochea waelekee kwenye ndoa za utotoni na huo unahesabika ni ukatili wa kijinsia.

Ni kweli, hilo analolisema halipo Songwe peke yake, ila limetawanyika katika maeneo mengi sana na hasa vijijini.

Kwa mtazamo na uzoefu wangu, ni afadhali mjini ambako kuna mwamko na watu wana hofu ya mkono wa sheria, kwa sababu vyombo vya serikali na dola vipo karibu na vinaangaza.

Mara zote vyombo hivyo vinaponusa uovu, basi havifumbii macho. Tatizo vijijini bado kuna baadhi ya utamaduni mbaya unaoendelea kutekelezwa hadi sasa na ndiyo maana, hata ikitokea hali kama hiyo uongozi wa kijiji unafumbia macho, kwa sababu baadhi yao wanaamini kwenye hilo.

Huwa najiuliza, hivi kweli watu hao wanakuwa wanawaza nini? Kwa kifupi mimi hapa nawaingiza na wanaume kwenye sakata hili pia.

Kwanza, wao ndiyo wanaokwenda kuwaoa mabinti ambao ni wanafunzi. Pia, waume za hao wanawake nao wanahusika, kwani kwa mujibu wa utamaduni wetu Waafrika kwa sehemu kubwa, ni kwamba wanaume ndiyo waamuzi wa mwisho katika yanayotuhusu.

Kama baba huyo hataki mtoto asiolewe ni kweli haolewi na kama anataka asome atasoma. Ni kweli diwani 'amewachana' wanawake wenzake, lakini hapo kwa asilimia kubwa wanaume nao wanahusika, kwa sababu inaonekana wanabariki matendo ya wake zao.

Huo utamaduni nadhani sasa umepitwa na wakati. Zamani wazazi walikuwa wanajitahidi tu kusomesha wanaume na kuwaacha mabinti nyumbani. Madai ni kwamba, mwanaume ndiyo anatakiwa asome ili ajitegemee, apate kazi na awe na familia yake aweze kuihudumia.

Lakini, dhana ikabaki mwanamke yeye ni mtu wa kuolewa hata kama hajasoma, atamtegemea mume kwenye maisha yake, akimtunza na kumjali kwa shida na raha.

Kwa sasa hilo lipo, lakini likibeba mageuzi makubwa na sura mpya. Wanawake wanaolewa kwa sababu ni jambo la heshima na utaratibu wa maisha, ikiwa ni mahitaji ya kibinadamu, pia kiimani.

Siku hizi wanawake nao wanatunza hata wanaume.

Kwa miaka ya karibuni, kuna mageuzi dunia nzima kuhusu wanawake na wanaume.

Wanawake wamesoma, wamejiendeleza, wamekuwa wafanyabiashara wakubwa na akili kubwa kwenye uongozi pengine hata kuwapiku wanaume.

Kinamama hao, hata katika mfano wa uongozi kitaifa sasa wameshika usukani, hata kurudi kwa walioko shule ngazi ya msingi hadi vyuoni, wanaongoza kwenye matokeo ya ufaulu.

Huo unafaa kuwa mwongozo kwetu sote na hasa wazazi kuondokana na imani za kutosomesha wanawake, kwani wameonekana wanaelimika vizuri zaidi na hata kuzaliwa viongozi bora.

Wazazi wasiwe na tamaa ya mali za mapema. Mali ambazo wanapewa mara moja na kumalizika, huku binti akiendelea na mateso kwa mume.

Uchunguzi wangu mdogo tu kwenye jamii, nimegundua pia watoto wa kike ndiyo wanaowasaidia zaidi wazazi wao wanapoelimika au kuwa na kipato chao kuliko wa kiume.

Sina maana watoto wa kiume wasisomeshwe, la hasha, lakini ukweli ni kwamba wanaume wanapokuwa na pesa, husaidia au hutoa zaidi upande wa mke, yaani ukweni kuliko kwao kwa wazazi wake.

Lakini, wanawake msaada wao hupelekwa zaidi kwa wazazi wake. Hilo ni somo dogo nawapa wazazi kuwa kumsomesha mtoto wa kike ni kama vile umejiwekea akiba isiyooza.

# Jela miaka 20 kwa kukutwa na jino la ngiri la dola 450

**Na Ibrahim Yassin,** MBOZI

NDAMO Mathius (19), mkazi wa Kata ya Mkwajuni wilayani Songwe mkoani hapo, amehukumiwa kifungo cha miaka 20 jela na kulipa faini ya Sh. milioni 3 kwa tuhuma za kukutwa na jino la ngiri.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Mbozi, Nemes Chami, baada ya kukutwa na hatia ya kukutwa na jino hilo ambalo ni nyara ya serikali yenye thamani ya dola 450 za Marekani.

Awali ilidaiwa mahakamani huko na Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Pasco Manawa, kuwa Oktoba 17, 2021 mshtakiwa alikamatwa na jino hilo la ngiri, jambo ambalo ni kinyume cha sheria, lakini mshtakiwa alikana kutenda kosa hilo.

Akijitetea mahakamani huko wakati wa hukumu, mshtakiwa alikiri kutenda kosa hilo na kuiomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa hana ndugu wa kumsaidia kutokana na baba yake ameshafariki dunia na mama yake ni mlemavu wa viungo. "Mheshimiwa hakimu, ni kweli nilitenda kosa hilo, lakini ninaomba mahakama yako tukufu inipunguzie adhabu kutokana na mimi kuwa sina ndugu, baba yangu alishafariki dunia na mama yangu ni mlemavu ananitegemea," alijitetea.

Licha ya utetezi huo, Hakimu Chami alisema mahakama imezingatia katiba, sheria na kununi ya rasilimali za serikali, hivyo mahakama inamtia hatiani mshtakiwa kutokana na kosa alilotenda kwenda jela kifungo cha miaka 20 na faini ya Sh. milioni tatu.

"Mahakama hii pasipo kuacha shaka, imejiridhisha na ushahidi uliotolewa mahakamani, hivyo utakwenda kutumikia adhabu hiyo ya miaka 20 jela na kulipa faini ya Sh. milioni tatu ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama hiyo," alisema.

Nje ya mahakama, Asajile Mbembela mkazi wa Mbozi, alipongeza hukumu hiyo, akiamini vijana wataacha tabia ya kutafuta mali kwa njia za mkato.



Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martin Shigela (kulia), akisikiliza jambo kwa Meneja Upokeaji Tumbaku Mbichi, Elizaberth Chuma (katikati), alipotembelea kiwanda cha kusindika tumbaku cha Alliance One Tobacco Tanzania Ltd, Kingolwira mkoani humo juzi. Kushoto ni Mkurugenzi wa Kiwanda hicho, Guy Mc Donald. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni yamwaga bil. 86/- kwa wakulima wa tumbaku

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

KAMPUNI ya ununuzi na usindikaji tumbaku nchini ya Alliance One Tobacco Tanzania Ltd (AOTTL) yenye makao makuu yake mjini Morogoro, imelipa Sh. bilioni 86 kwa wakulima ilioingia nao mkataba kwa msimu wa zao hilo kwa mwaka 2022.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Ephraim Mapoore, alibainisha hayo juzi wakati akimpa taarifa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martin Shigela, aliyezuru kiwandani huko ili kuzindua msimu wa uchakataji wa zao hilo.

Alisema wamelipa fedha hizo baada ya kununua kilo milioni 22 za tumbaku kutoka kwa wakulima 11,000 ambao wanatoka katika vyama vya msingi vya wakulima zaidi ya 150.

"Tumelipa zaidi ya Sh. bilioni 86 kwa wakulima hao 11,000 kutoka maeneo mbalimbali yanayolima tumbaku nchini. Kama kampuni, tumedhamiria kuona tunabadili maisha ya wakulima wetu na familia zao," alitamba.

Mkurugenzi huyo pia alisema kwa kipindi cha miaka mitano, kampuni imetumia Sh. bilioni 26.5 kama mishahara na marupurupu mengine kwa wafanyakazi wake.

Kampuni hiyo ina wafanyakazi wa kudumu 350 na huajiri wengine 3,000 wakati wa msimu wa tumbaku.

AOTTL ambayo ni kampuni tanzu ya Alliance One International (AOI) yenye makao makuu yake North Carolina, Marekani, pia katika miaka mitano iliyopita kila mwaka imekuwa ikilipa kodi mbalimbali zinazohusiana na ajira Sh. bilioni 11.6 na kupeleka katika mifuko ya hifadhi ya jamii Sh. bilioni 1.718 kila mwaka.

Mkurugenzi huyo alisema kampuni inasaidia katika kuinua Pato la Taifa kwa kuchangia asilimia tatu ya tozo inazotakiwa kulipa katika wilaya inakonunua tumbaku, kukamilisha tozo ya hifadhi kwa vyama vya msingi ya dola 0.07 kwa kila kilo ya tumbaku iliyonunuliwa huku tozo kwa vyama vikuu vya ushirika vya WETCU, LACTU, KATCU na CETCU zikilipwa dola za Marekani 0.023 kwa kila kilo iliyonunuliwa.

Alisema kampuni hiyo imejikita katika kusaidia jamii maeneo mbalimbali ikiwamo ufadhili wa mbio za Mwenge wa Uhuru katika wilaya 15 ambazo ipo na kusaidia Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro vifaa tiba, kukabiliana na janga la UVIKO-19 pamoja na kukarabati na kujenga shule mbalimbali mjini hapa.

Pamoja na mafanikio yote hayo, mkurugenzi huyo alitaja vikwazo kadhaa vinavyowakabili ikiwamo umeme usiokuwa wa uhakika ingawa wanalipa Sh. bilioni 1.4 kila mwaka kwa Shirika la Umeme (TANESCO) kwa ajili ya kupatiwa nishati hiyo.

Alibainisha kuwa asilimia 31 ya matumizi ya umeme katika kiwanda chake inatokana na nishati inayofuliwa na jenereta lake na hivyo TANESCO kukosa mapato.

"Kuna tatizo la maunganisho ya maji kutoka MORUWASA kwenda kiwandani na pia kuwapo na kodi nyingi ambazo zimesababisha gharama kuwa juu kwa asilimia 30," alisema.

Mkurugenzi huyo pia alisema wamekuwa na mzozo na Mamlaka ya Mapato (TRA) kuhusu masuala mbalimbali ya ulipaji wa kodi.

Mkuu wa Mkoa Shigela alipongeza kampuni hiyo kwa juhudi kubwa inazofanya kuboresha maisha ya wakulima wa tumbaku na wafanyakazi wake tangu waanze shughuli zao mwaka 1998.

Alisema ziara yake kiwandani huko ni kutekeleza maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kutaka wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kuhakikisha wanatembelea wawekezaji na kutatua matatizo yao.

Alihakikishia wawekezaji hao kwamba tatizo lao la umeme na maji litatuliwa haraka.

Pia aliahidi kuzungumza na maofisa wa TRA kuona ni namna gani wanaweza kufikia mwafaka kuhusu masuala ya kodi kwa kuangalia pia agizo la Rais Samia alilolitoa hivi karibuni alipokuwa katika ziara ya Mkoa wa Kagera.

"Ni vyema tukasaidia viwanda hivi na kuhakikisha wanaongeza tija kutoka kuchakata kilo milioni 70,000 hadi zaidi ya kilo milioni 150,000," alisema Shigela.

AOTTL ilianzishwa nchini mwaka 1998 baada ya kuungana kwa DIMON Incorporated na Standard Commercial Corporation (STANCOM), zote za Marekani.

## Bunge lakunwa na miradi ya TANAPA

**Na Somoe Ng'itu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imepongeza juhudi zinazofanywa na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) katika kuhakikisha miradi ya uboreshaji miundombinu inafanyika kwa ubora na kwa wakati.

Kamati hiyo imeeleza kuridhishwa na mwenendo wa miradi hiyo ilipotembelea Hifadhi ya Taifa Tarangire kukagua miradi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Daniel Sillo, alisema TANAPA chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii inastahili pongezi kwa kazi nzuri ya kusimamia miradi hiyo sanjari na maboresho wanayoyafanya ambayo yanakwenda kukuza uchumi wa taifa.

"Tunaamini mkiboresha miundombinu yote, italeta tija na kwa kiasi fulani itachangia kuongeza pato na kukuza uchumi wetu," alisema.

Sillo aliwataka watendaji wa TANAPA kuendelea kusimamia miradi yote kwa uadilifu na kila mmoja atimize wajibu wake ili kuzidi kuwa chachu ya mafanikio.

Akizungumza kwa niaba ya Kamishna wa Uhifadhi – TANAPA, William Mwakilema, Kamishna Msaidizi anayeshughulikia uendelezaji wa Hifadhi za Taifa, Paul Banga, alisema zaidi Sh. bilioni 46 zilitengwa kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ambazo Hifadhi ya Taifa Tarangire ilipata Sh. bilioni 2.7 zilizotumika kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege na matengenezo ya barabara na vivuko.

Miradi mingine inayotekelezwa na fedha hizo ni pamoja na ujenzi wa madaraja, barabara na njia za kupanda milima, eneo la kutua helikopta za uokozi, ujenzi wa malango ya ukusanyaji mapato, ununuzi wa mitambo na magari pamoja na ufungaji wa mifumo ya ufuatiliaji wa magari na mitambo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya TANAPA, Jenerali mstaafu George Waitara, alisema miradi hiyo imekamilika ndani ya muda na kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia kutoa fedha za UVIKO – 19 ili kuinua sekta ya utalii.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, aliwaahidi wajumbe wa kamati hiyo ya Bunge kuwa miradi yote inayotekelezwa chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii inakamilika ndani ya muda uliopangwa.

Moja ya hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu sekta ya utalii katika ripoti yake kwa mwaka 2020/21, ni serikali kusuasua kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyo chini ya TANAPA.

# Rais aridhia msamaha riba wadaiwa sugu kodi ya ardhi

**Na Munir Shemweta,**
SERENGETI

RAIS Samia Suluhu Hassan ameridhia msamaha wa riba ya kodi ya pango la ardhi kwa wadaiwa sugu kwa masharti kwamba wawe wamelipa madeni ya msingi ndani ya miezi sita kuanzia mwezi huu.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alibainisha hayo juzi katika mkutano na wananchi wa kijiji cha Nyachoka, Serengeti mkoani Mara wakati wa kukabidhi hati miliki za kimila.

Hatimiliki za kimila 6,155 zimekamilika na kutolewa kwa wananchi wa vijiji 22 katika Wilaya ya Serengeti. Kati ya hizo, hati 1,621 sawa na asilimia 26 zimekamilishwa kwa ajili ya kinamama na 1,519 sawa na asilimia 25 ni za umiliki pacha kati ya wanaume na wanawake.

Dk. Mabula alisema yeye pamoja na Waziri wa Fedha na Mipango ambaye ndiye mwenye dhamana ya kusamehe, watakutana na kupanga namna bora ya kutekeleza msamaha huo.

"Najua kuna wengi wanadaiwa madeni ya muda mrefu kwa hiyo kumetokea msamaha kuanzia Julai mpaka Desemba, mwaka huu. Watakaoweza kulipa ndani ya miezi hii sita, wale ambao madeni yao yana miaka mitano kurudi nyuma watalipa bila ile tozo ya riba.

"Mheshimiwa Rais (Samia) ameridhia kupitia Waziri wa Fedha na Mipango (Dk. Mwigulu Nchemba) kwa kushirikiana na Waziri wa Ardhi waweke utaratibu mzuri wa ninyi kuondolewa tozo ile na msamaha ni wa miezi sita tu. Kama una ndugu mpigie simu mwambie serikali imetoa msamaha kwa wadaiwa sugu ili watoke katika jina baya la wadaiwa sugu," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, mmiliki wa ardhi atakayeshindwa kulipa madeni yake katika kipindi hicho, atadaiwa madeni yake pamoja na riba na akishindwa kufanya hivyo atafikishwa kwenye vyombo vya sheria ambako huko uamuzi wake ni kulipa au kunyang'anywa ardhi anayoimiliki.

Kuhusu utoaji hatimiliki za kimila, Dk. Mabula alisema, hatua ya kumilikishwa ardhi kwa nyaraka kuna faida kubwa katika maisha ya kila siku ikiwamo usalama wa ardhi, uhakika wa miliki, kupunguza migogoro na nyaraka hiyo kutumika kama dhamana. Zaidi ya wananchi 6,000 katika vijiji 22 wamepangiwa matumizi bora ya ardhi katika maeneo yao na kuwekewa mipaka ya kudumu ili kuepuka migogoro ya mipaka kwenye ardhi zao.

Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, Shirika la Hifadhi la Taifa Serengeti (SENAPA) na Shirika la Frankfurt Zoological Society (FZS) kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) kupitia mradi wa utunzaji na uendelezaji wa Ikolojia ya Serengeti waliingia makubaliano ya pamoja kwa ajili ya kuwezesha uandaaji wa mpango wa matumizi ya ardhi ya vijiji vinavyopakana na maeneo yaliyohifadhiwa yanayounda ikolojia ya serengeti inayojumuisha hifadhi za taifa na mapori ya akiba.

Madhumuni ya mradi huo ni pamoja na kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi kati ya vijiji na eneo la hifadhi, kutatua migogoro ya mipaka kati ya maeneo ya kiutawala na kutoa elimu ya uhifadhi na sheria mbalimbali zinazosimamia mipango ya matumizi ya ardhi nchini.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (kulia), akikabidhi kitabu cha mpango wa matumizi ya ardhi kwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyichoka, wilayani Serengeti Mkoa wa Mara, Imanuel Cairo Sochora, wakati wa kukabidhi hati miliki za kimila juzi. **PICHA: WANMM**

## WMA yaonya wizi wa vipimo

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

WAKALA wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Iringa imewataka wadau wote wa mazao ya kilimo kujiepusha na udanganyifu hasa uchakachuaji wa mizani wakati wa ununuzi wa mazao shambani.

Pamoja na kutoa wito huo, WMA imeonya kwamba yeyote atakayekamatwa kwa makosa hayo atashtakiwa kwa mujibu wa sheria.

Onyo hilo lilitolewa juzi wakati wa mwendelezo wa utoaji elimu kwa wakulima, wadau na wafanyabiashara wakati huu wa mavuno ili kuhakikisha vipimo sahihi vinatumika wakati wa kuuza mazao ili kukuza uchumi wa mkoa na taifa kwa jumla.

Kaimu Meneja wa WMA Mkoa wa Iringa, Lina Msuya, alisema lengo la elimu hiyo kwa wakulima kuhusu mizani sahihi ni kumlinda mkulima ili apate fedha anayostahili kulingana na uzito wa mazao anayoiuza.

Pia alisema lengo lingine ni kuhakikisha mkulima anajua mambo muhimu ya kuzingatia ili kumwezesha kutambua mizani sahihi na iliyohakikiwa pamoja na kutambua kwa urahisi mizani zilizochezewa au kuharibiwa.

Alisema baada ya elimu hiyo, wakulima wa mazao mbalimbali watakuwa na uwezo wa kutambua mizani iliyohakikiwa na WMA kwa kuzingatia lakiri yenye ngao ya taifa na tarakimu mbili za mwisho wa mwaka husika ambazo kwa mwaka 2022 itasomeka 22.

Pia mizani iliyohakikiwa itakuwa na stika maalum ya WMA ambayo inaonyesha tarehe mizani iliyokaguliwa na tarehe ya mwisho kutumika. Vilevile mkulima anatakiwa kuhakikisha kuwa mizani inasoma sifuri (0) kabla hajaweka mazao yake kwa ajili ya kuyapima.

# Majitaka yatumika kutengeneza mbolea

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), imebuni utengenezaji wa mbolea ya mashambani kwa kutumia tope kinyesi.

Mamlaka hiyo ina mtambo wa kutibu na kuchakata tope kinyesi (majitaka) ulioko maeneo ya Nhelegani Kata ya Kizumbi Manispaa ya Shinyanga, ambao hutumika kusomba majitaka kwa mji wote wa Shinyanga na kuhifadhi mahali hapo na kuweka mazingira kuwa safi.

Mkurugenzi Mtendaji wa SHUWASA, Mhandisi Yusuph Katopola, alibainisha hayo juzi wakati wajumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA) walipotembelea mtambo huo wa kutibu na kuchakata tope kinyesi.

Alisema SHUWASA kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV), ilibuni namna ya kugeuza tope hilo kinyesi kuwa mali, ndipo wakaona wazalishe mbolea ambayo itatumika mashambani na kuongeza mavuno kwa wakulima.

"Mtambo huu wa kutibu na kuchakata tope kinyesi ulianza kufanya kazi Juni, mwaka jana na uzalishaji huu wa mbolea itokanayo na kinyesi tumeianza muda si mrefu. Lengo letu ni kuzalisha mbolea nyingi na kutatua uhaba wa mbolea hapa nchini," alisema Katopola.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya AUWSA, Dk. Jackline Mkindi, alisema wamefanya ziara SHUWASA ili kujifunza jinsi gani wanavyofanya kazi, pamoja na kutibu tope kinyesi hadi kuwa bidhaa.

Alisema kilimo ndiyo njia sahihi ya kuwekeza na SHUWASA imefanya jambo sahihi la kuzalisha mbolea kwa kutumia majitaka ambayo itasaidia kupunguza uhaba wa mbolea nchini.

Dk. Mkindi aliitaka SHUWASA isilichukulie jambo hilo poa bali kuingia ubia endelevu na sekta binafsi ambayo wamewekeza kwenye mbolea ili wazo hilo la kimkakati lisonge mbele na kuongeza kasi ya uzalishaji wa mbolea.

# Wadau wasisitizwa kulinda Ziwa Victoria

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imewataka wadau mbalimbali kuendeleza jitihada za kulinda Ziwa Victoria dhidi ya uchafuzi kutokana na umuhimu wake kwa shughuli za maendeleo ya watu barani Afrika.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, alisema hayo juzi Dar es Salaam wakati akizindua Mpango Mkakati wa Kusimamia Mazingira katika Ziwa Victoria.

Mpango huo unaratibiwa na Kituo cha Sayansi ya Mazingira (Center for Science Environment- CSE) cha India ambacho kimekuwa kikitafiti chanzo cha uchafuzi wa ziwa hilo na kutafuta majibu yake.

Waziri Jafo alisema kituo hicho kimekuwa msaada mkubwa kwenye ulinzi na usafi wa Ziwa Victoria ambalo limekuwa tegemeo kubwa kwa mamilioni ya watu wa Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Alisema ziwa hilo limekuwa chanzo kikubwa cha maji ya Mto Nile ambao unategemewa na zaidi ya watu milioni 40 kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi hasa kilimo na uvuvi.

"Hili ziwa ni kubwa sana na linategemewa zaidi duniani kwa sababu maji yake ndiyo uchumi wa wenzetu. Kwa hiyo ninapoona wadau kama nyinyi mnajitokeza kulilinda inanipa moyo sana, wenzetu Misri wanategemea sana Mto Nile ambao unapata maji kupitia Ziwa Victoria," alisema.

Jafo alisema amefarijika kuona wageni wametembelea ziwa hilo na kukuta halijachafuliwa kama ambavyo imekuwa ikitokea hasa wakati wa kipindi cha mvua, hivyo akataka hali hiyo ya usafi iwe endelevu.

"Ukitembelea Ziwa Victoria msimu ambao hauna mvua, unaweza kudhani kwamba hali ndivyo ilivyo siku zote. Lakini mvua zikianza ndipo utaona hali halisi ya mazingira yake. Wageni wetu wameenda wamekuta safi, sasa hali hii iendelee hata msimu wa mvua," alisema.

Jafo pia alipongeza ushirikiano uliopo baina ya serikali ya Tanzania na India ambayo alisema kwa sasa inafadhili miradi 28 ya maji yenye thamani ya zaidi ya Sh. trilioni moja kwenye mikoa mbalimbali nchini na tayari imeshaanza kujengwa.

"Serikali ya India inatusaidia sana kwenye mambo mengi sasa ninapoona na ninyi mmekuja kutusaidia kulinda Ziwa Victoria dhidi ya uchafuzi wa mazingira yake, inazidi kunipa amani ya moyo kwamba ninyi ni ndugu zetu na mnapenda maendeleo yetu," alisema.

Mkurugenzi wa CSE, Dk. Sunita Narain, alipongeza jitihada zinazofanywa na serikali kulinda na kuhifadhi mazingira na kwa namna ambavyo kituo hicho kimepata mapokezi mazuri.

"Tunaishukuru serikali ya Tanzania kwa kutupokea vizuri tangu tulipofika nchini mwezi uliopita, tumetembelea Ziwa Victoria kujionea hali ilivyo na tumeridhika kwa namna mikakati inavyowekwa kulilinda dhidi ya uchafuzi," alisema Dk. Suniti. Naye Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, alisema baraza limekuwa na ushirikiano wa karibu na CSE.

Alisema wanashirikiana katika kuandaa shughuli mbalimbali za kimazingira ikiwa ni pamoja na uandaaji wa Mpango Mkakati wa Usimamizi wa Mazingira kwa Ziwa Victoria na kwamba uandaaji wa mpango huo umezingatia miongozo mbalimbali ya nchi.

"Uanzishaji wa makakati ni jitihada za baraza katika utekelezaji wa Mkakati Kabambe wa Mazingira wa Taifa wa Mwaka 2022/32 uliozinduliwa rasmi Juni ,2022 na pia Ajenda ya Taifa ya Utafiti wa Mazingira (2017/22)," alisema Dk. Gwamaka.

## Wataka pembejeo kupitishiwa Amcos

**Na Julieth Mkireri,** KIBITI

SERIKALI kupitia Wizara ya Kilimo imeombwa kurudisha utaratibu wa kupeleka pembejeo za korosho kwa vyama vya msingi (AMCOS) badala ya ilivyo sasa zinavyogawiwa kupitia serikali za vijiji.

Ombi hilo limetolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Krenk Agro ya Kibiti inayosimamia maghala, Remigeous Kailembo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari mjini hapo.

"Maoni yangu ingekuwa vizuri pembejeo zingekuwa zinagawiwa kwa AMCOS ambao wanajua wakulima wao badala ya utaratibu wa kugawa kwenye serikali za vijiji," alisema.

Kailembo alisema vyama vya ushirika ndio vinavyowatambua wakulima waliosafisha mashamba ya wakulima, hivyo wakipewa jukumu la kugawa pembejeo zitawafikia walengwa kwa wakati.

"Pembejeo zinapofikishwa kwenye serikali za vijiji, wengi wanaopatiwa ni wale wenye mashamba ya asili ambao baadhi yao waliyakodisha, hivyo wanapopewa pembejeo baadhi yao wanauza na walengwa kukosa pembejeo," alisema.

Aliipongeza serikali kwa kuwahisha pembejeo hizo kwa wakulima ambapo zikiwahishwa kwa walengwa uzalishaji utaongezeka.

Pia aliwashauri wakulima wa zao la ufuta ambao bado hawajapeleka ufuta ghalani kufanya hivyo ili uingie kwenye minada inayoendelea na kutaka mikoa mingine kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani ambao umekuwa mkombozi kwa wakulima.

Katibu wa Chama cha Ushirika (AMCOS) cha Kibiti, Abdallah Kigumi, alisema awali pembejeo zilikuwa zikigawiwa kwenye serikali za vijiji lakini baadaye ikabadilishwa na kugawiwa kwenye AMCOS na kwamba utaratibu kwa mwaka huu umebadilishwa na kurudi kwenye serikali za vijiji.

Kigumi alisema utaratibu huo unaofanyika mwaka huu umekuwa kikwazo kwa wakulima wengi ambao bado hadi sasa hawajapata na hivyo kuendelea kuulizia kwenye vyama vyao vya ushirika.

Katibu huyo aliomba serikali kuongeza pembejeo ili zitosheleze wakulima na kuongeza uzalishaji.

Mmoja wa wakulima, Seleman Mussa, aliiomba serikali kurejesha utaratibu wa pembejeo kwenye AMCOS ili wapate kwa urahisi.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Buriani (wa pili kushoto), akipokea msaada wa madawati 100 kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Mikopo Benki ya Exim, Zainabu Nungu (wa tatu kulia), uliyotolewa na benki hiyo, mkoani humo jana, ili kusaidia jitihada za mkoa huo kukabiliana na changamoto ya uhaba wa madawati. Wanaoshuhudia ni Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Dk. Yahaya Nawanda (kushoto), Katibu wa CCM wa Mkoa huo, Solomon Kasaba (wa pili kulia) na Ofisa Elimu wa mkoa huo, Juma Kaponda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Exim yatoa msaada madawati 100

**Na Mwandishi Wetu,** TABORA

BENKI ya Exim Tanzania imekabidhi msaada wa madawati 100 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 20 mkoani Tabora ikiwa ni mwendelezo wa mkakati wake wa kutoa msaada wa madawati 1,000 katika mikoa mbalimbali nchini.

Msaada huo wa madawati ni mwendelezo wa kuchangia maendeleo ya elimu bora kupitia mpango wake wa uwajibikaji kwa jamii (CSR) ujulikanao kama Exim Cares.

Madawati hayo yalikabidhiwa na Mkuu wa Kitengo cha Mikopo ya Exim, Zainabu Nungu, kwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Buriani, wakati wa hafla fupi iliyofanyika kwenye ofisi ya mkuu wa mkoa jana.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Balozi Buriani pamoja na kuishukuru Benki ya Exim, alisema msaada huo unakwenda sambamba na jitihada za serikali za kuboresha hali ya elimu mkoani hapa na kwamba utasaidia kupunguza uhitaji wa madawati uliotokana na miradi mingi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa.

"Msaada huu utasaidia kupunguza uhaba wa madawati katika baadhi ya shule zetu. Tunashukuru sana wenzetu wa Benki ya Exim kwa msaada huu na tunaomba mwendelee kusaidia kwenye maeneo mengine ikiwamo sekta ya afya.

"Mheshimiwa Rais anapambana kutafuta fedha kwa ajili ya miradi mikubwa inayoendelea nchini, hivyo ni jambo linalotia moyo kwake kuona wadau kama benki mkiendelea kumuunga mkono," alisema.

Aidha, Balozi Buriani alizitaja baadhi ya shule zitakazonufaika na msaada huo kuwa ni baadhi ya shule zilizoko katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ambazo zinazokabiliwa na uhaba mkubwa wa madawati.

Kwa upande wake, Nungu alisema benki hiyo imejitolea kusaidia kuboresha ustawi wa jamii kupitia misaada ya kijamii ikiwamo elimu na kwamba wamegeuswa na changamoto ya madawati kwenye baadhi ya maeneo nchini, hivyo kuwafanya kuchukua hatua hiyo ili kuboresha sekta hiyo muhimu.

"Ni furaha kwetu kuwa sehemu ya kutatua changamoto kwenye sekta muhimu kama hii. Huu ni mwendelezo tu bado tunaendelea na mikoa mingine kwa kuwa lengo ni kutoa msaada wa madawati 1,000 kama tulivyoahidi wakati tunazindua mpango huu mwishoni mwa mwaka jana," alisema.

Mbali na Tabora, Nungu alisema benki pia imetoa msaada wa madawati katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Lindi, Shinyanga na Mwanza.

# Serikali kuendeleza nguvu kutangaza Kiswahili

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Fatma Rajabu, amesema wizara imejipanga kuongeza nguvu ya kutangaza lugha ya Kiswahili katika mataifa mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), alisema bado kunahitajika kuongeza nguvu ya kutangaza Kiswahili duniani.

"Balozi zetu zilizopo nje ya nchi zimefanya jitihada kubwa kutangaza fursa mbalimbali zilizopo nchini na hii imechangia ongezeko kubwa la wafanyabiashara kuja kwenye maonyesho hayo.

Alisema kupitia maonyesho hayo, wizara hiyo imeendelea kutangaza diplomasia ya uchumi.

Pia alisema wizara hiyo itaendelea kutangaza utalii kwa kupitia filamu ya Royal Tour ambayo imeanza kuonyesha matokeo chanya katika sekta ya utalii nchini.

Alisema katika kuinua diplomasia ya uchumi, wanatarajia kushirikiana na Wizara ya Kilimo ili iwashawishi wakulima kulima mazao ambayo yatauzwa nje ya nchi.

"Kwa sasa tuna soko kubwa la maharagwe ya soya, mafuta nchini China na hivi karibuni nchi ya Saudi Arabia itaanza kupokea nyama kutoka Tanzania," alisema Balozi Fatma.

Aliwashauri wafanyabiashara na wakulima kuendelea kutumia tovuti ya wizara hiyo ili kujionea fursa mbalimbali zinazopatikana katika nchi mbalimbali.



Mwananchi akiwa amebeba boksi lenye bidhaa katika maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam yanayosimamiwa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), barabara ya Kilwa jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Zaidi ya 700 wapata elimu utumiaji usafiri ardhini

ZAIDI ya watu 700 wamepata elimu ya haki na wajibu ya utumiaji wa vyombo vya usafiri ardhini kutoka kwa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC), katika maonyesho ya 46 ya biashara.

Akizungumza na Nipashe, Mkuu wa Idara ya Fedha na Utawala, Fatuma Kulita, alisema pia walitumia maonyesho hayo kutoa elimu ya ukataji wa tiketi kwa njia ya mtandao ambayo tayari imeanza kutumika tangu Julai mosi mwaka huu.

"Tupo pamoja na serikali katika kuhimiza wananchi na kuwapa elimu wafahamu faida ya ukataji tiketi kwa njia ya mtandao," alisema Fatuma.

Alisema licha ya kutoa elimu hiyo ya kukata tiketi kwa njia ya mtandao, pia waliwaelimisha kufahamu haki na wajibu wao wanapokuwa katika vyombo vya usafiri ardhini.

Pia, alisema LATRA CCC wamekuwa wakitoa elimu kwa klabu za wanafunzi wa shule za sekondari na msingi lengo ni kutaka jamii ifahamu kwa usahihi haki, wajibu na jinsi ya kukata tiketi kwa njia ya mtandao wanapotumia usafiri wa ardhini.

Alisema ukataji wa tiketi kwa njia ya mtandao unasaidia kupunguza usumbufu na kupoteza muda kwa wasafiri.

"Kutumia njia ya mtandao ni bora zaidi kwa sababu, kwanza hakupotezi muda wa kuhangaika mpaka kwenda ofisini, huu unakata mara moja na unaendelea na shughuli zako nyingine," alisema Fatma.

## Mkojo wa sungura unavyofukuza wadudu kwenye mboga

MWANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Mzumbe amegundua matumizi ya mkojo wa sungura katika kufukuza wadudu wanaoshambulia mboga na matunda.

Akizunguza na Nipashe kwenye banda la chuo hicho, mwanafunzi wa Sayansi ya Uzamili wa chuo hicho, Nelson Kissanga, alisema wamegundua mkojo wa sungura unaharufu kali na sio rafiki kwa wadudu hususani wale waharibifu katika mboga zenye jamii ya maua na matunda.

Kissanga alisema kugundua mfumo huo kutasaidia mimea ya wakulima kuwa salama na pia wameunga mkono kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa Tanzania ni mahali sahihi pa biashara na uwekezaji.

"Tumekuja na ubunifu huu ambao utasaidia wakulima kutopata hasara pindi wadudu watakapoingia katika bustani na mashamba yao kuharibu mboga na matunda," alisema Kissanga.

"Wadudu wengi huvutiwa sana na mvuto wa mboga na matunda kwa sababu hufuata harufu nzuri hasa yanapochanua, ni waharibifu katika mboga na hususani jamii ya maua pamoja na matunda."

Alisema mkojo huo wa sungura ni mbadala wa utumiaji wa kupuliza dawa katika mboga na matunda.

"Mkojo huo wa sungura ni fursa kwa watu wengi kwa sababu unapowafuga na kupata mkojo wao, mfugaji anapaswa kujenga banda la juu ili wanapokojoa kunakuwa na kinga," alisema Kissanga.

Alisema hauna shida yoyote kwa watumiaji kutokana na kutokuwa na kemikali na ni rafiki wa mazingira.

## Wavuvi, wakulima, wafugaji kupatiwa bima

KAMISHNA wa Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima nchini (TIRA), Dk. Baghayo Saqware, amesema wamejipanga kushirikiana na Shirika la Bima la Taifa (NIC) kuwafikia wakulima, wafugaji na wavuvi wote nchini ili kuwapatia bima kwa ajili ya biashara zao.

Dk. Saqware alisema hayo alipotembelea banda la NIC.

Alisema wameamua kushirikiana na NIC kuyafikia makundi hayo kutoka katika sekta hizo kutokana na umuhimu wake.

"Serikali imekuwa ikitegemea sana NIC katika kufikisha bima kwenye maeneo ya kilimo, majengo na mengine wamefanya kazi nzuri, kwa hiyo tumeona tuendeleze hii kazi waliyoianza ili kuhakikisha kwamba shughuli zinazofanywa kutoka kwenye makundi haya zinakuwa salama," alisema Dk. Saqware.

"Ukizungumzia bima Tanzania hakuna namna unaweza kuisahau NIC kwa maana ya wataalamu, uzoefu pamoja na mtaji, kwa hiyo tuna uhakika tunakwenda kufanya kazi nzuri."

Naye Mkurungezi wa Masoko na huduma kwa wateja NIC, Yesaya Mwakifulele alisema wananchi waliofika katika banda lao wamepata elimu kuhusu namna wanavyoweza kuipata bima kwenye masuala mbalimbali.

Pia, alisema kwenye maonyesho hayo walikuwa na programu mpya inayojulikana kama APP ya NIC kigajani ambayo inamwezesha mteja kupata huduma akiwa nyumbani bila ya kufika katika ofisi zao.

"Kupitia APP hiyo mteja anaweza kujihudumia kwa hatua chache tu ambayo ataweza kukata bima ya aina mbalimbali ikiwamo ya nyumba na gari," alisema Mwakifulele.

ama

ALHAMISI JULAI 14, 2022

AFYA NA MAZINGIRA



Wafugaji walia namna ukataji wa miti ovyo unavyofilisi uchumi wao

Ukurasa 12



KAMPENI ELIMU AFYA YA MTOTO... Ijue Programu ya Sayansi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo kwa Mtoto

Ukurasa 14

## KUFANIKISHA CHANJO UVIKO - 19...

# Waziri Ummy: Tumepiga hatua, lakini kuna kazi kubwa tuendako

**Na Yasmine Protace**

HADI sasa kitaifa vita inaendelea dhidi ya ugonjwa wa Corona, serikali ikijikita kupambana nayo kupitia chanjo zinazoendelea kutolewa nchini, katika vita vinavyojulikana kuwa mapambano ya kitaifa.

Hadi sasa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, amebainisha kuwa serikali kupitia Wizara ya Afya, imelenga kufikia asilimia 70 ya waliochanja, ni sehemu ya mkakati wa dunia wa kupambana dhidi ya ugonjwa UVIKO-19.

Waziri Ummy amebainisha hayo hivi karibuni, akiwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na Mwakilishi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, katika mkutano na Katibu Mkuu Msaidizi na Mratibu Mkuu wa Kimataifa wa Mapambano dhidi ya UVIKO-19 kutoka Umoja wa Mataifa, Ted Chaiban.

"Katika kikao hiki tumejadili kiundani mafanikio, changamoto na namna ya kuboresha Sekta ya Afya, na kama Serikali tumeridhia lengo la uchanjaji wa asilimia 70 ya watu wote duniani, ikiwa ni sehemu ya mapambano dhidi ya UVIKO-19," anasema Chaiban.

Katika hadhira hiyo aliyoambatana na wajumbe kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF), Waziri Ummy anasisitiza imethibitishwa chanjo hiyo kuwa kinga kamili dhidi ya UVIKO-19, ikielekezwa walau asilimia 70 ya watu wote kupata chanjo wawe salama.



kikoloni, ilivyoangukia hatima ya afya. **PICHA: MTANDAO.**

Anasema, hadi kufika Aprili 5 mwaka huu, watu milioni 8.5 walishapatiwa chanjo, akiweka wazi bado kuna kazi kubwa ya kufanya kuweza kuchanja watu waliobaki, hata kuwafanya Watanzania kuishi dhidi ya ugonjwa huo, mithili ya magonjwa mengineyo yaliyozoeleka.

Waziri huyo wa Afya anatoa wito kwa Watanzania kuendelea kujitokeza zaidi kupata Chanjo ya UVIKO-19, akiwataja walio hatarini zaidi ni jamii ya wazee, wenye sugu kama vile shinikizo la damu, kisukari, saratani na Ukimwi.

Pia, Waziri Ummy ameendelea kusisitiza kuwa, chanjo ya UVIKO-19 inatolewa kwa hiari, ingawa anawaelekeza watoa huduma za afya, kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kwa hiari wakapate chanjo hiyo.

Waziri Ummy anatumia hadhira hiyo kuendelea kupiga marufuku tabia za watoa huduma, kulazimisha wananchi wanaoenda kupata huduma kuchanja kwa lazima na kusema kuwa tabia hiyo, ni kinyume cha miongozo na maadili ya taaluma za watoa huduma.

Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI, Innocent Bashungwa, anasisitiza kuwa itaendelea kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Afya, katika kusimamia uboreshaji huduma za afya nchini.

Aidha, Waziri Bashungwa anamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa dhamira yake kuifungua nchi na kukuza ushirikiano unaosaidia katika mapambano dhidi ya magonjwa mbalimbali, ikiwemo ugonjwa wa UVIKO-19.

Katibu Mkuu Msaidizi na Mratibu Mkuu wa Kimataifa wa mapambano dhidi ya UVIKO-19 kutoka Umoja wa Mataifa, Ted Chaiban, anampongeza Rais Samia Suluhu Hassan, akionyesha mfano kwa vitendo katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo kwa kupata chanjo dhidi ya ugonjwa huo.

Pia, anatoa wito kwa serikali kupitia Wizara ya Afya kuendelea na kasi ya utoaji elimu na uhamasishaji wananchi wakubali kupata chanjo hiyo, vilevile akiipongeza kwa jitihada za kuongeza idadi ya waliochanja ndani ya muda mfupi, kutoka asilimia 6.3 hadi asilimia 12.4.

MAZINGIRA

# Wafugaji walia namna ukataji wa miti ovyo unavyofilisi uchumi wao

## •Misitu yasambaratishwa, mifugo inatangatanga
## •Ni makazi yatokanayo na Operesheni Vijiji, 1974

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa Bagamoyo.**

UKATAJI miti kiholela unaotumika kutengeneza mkaa katika kijiji cha Chamakwezi wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani ulivyowaathiri wafugaji na kujikuta wakihamisha mifugo yao, kutokana na uharibifu wa mazingira.

Kijiji hicho kina idadi ya wakazi 4,712 ambao asilimia 90 ni wafugaji wanaoishi katika vitongoji vitano vya Chamakwezi yenyewe, Mjimwema, Idara ya Maji, Njiapanda na Mbala.

Ukataji miti kiholea unaendelea kuwa chanzo kikubwa cha mabadiliko ya hali ya hewa duniani, hasa kupanda kwa kiwango cha joto na kusababisha uharibifu wa mazingira.

Baadhi ya wakazi katika kijiji hicho wamelalamikia ukataji miti uliokithiri katika kijiji hicho na kusababisha athari kubwa katika mifugo yao, ikiwemo kufa kwa kukosa chakula na mazingira kutokuwa salama.

Malalamiko mengine inahusu pia uharibifu wa mazingira katika eneo hilo, mifugo inakosa chakula, hali iliyosababisha kuwahamisha kwenda maeneo mengine kutafuta nyasi.



Mwenyekiti wa Kijiji cha Mbala, kilichopo wilayani Bagamoyo, Lepa Mumbi akionyesha hali ya uharibifu wa misitu. **PICHA: BEATRICE SHAYO.**

**HISIA ZA WANAKIJIJI**

Jacob Samweli, mkazi wa kijiji hicho anasema kijiji cha Chamakwezi ni cha wafugaji na kiliundwa kutokana na Operesheni ya Vijiji vya Ujamaa kati ya mwaka 1974 hadi 1975, wafugaji waliondolewa katika maeneo tofauti na serikali ikawaleta katika eneo hilo kuendelea na shughuli zao.

Anasema, wakulima nao waliondolewa katika kijiji hicho wakapelekwa katika maeneo mengine na serikali iliwatengenezea majosho wakawa wanafanya shughuli zao vizuri za ufugaji.

Samweli anaeleza, ukataji miti katika eneo hilo, umewafanya wajikute wanapata madhara hasa kwa mifugo kushindwa kupita, kutokana na kuwepo miba mingi na uharibifu wa mazingira unaoendelea kuchukua nafasi, jambo linalowasumbua.

"Tunaathirika. Hali ya kijangwa zamani kulikuwa na misitu mingi na miti mikubwa, ila kwa sasa miti hakuna, kumekuwapo jangwa. Kutokana na mazingira hayo, mifugo tumeihamisha kuipeleka maeneo mengine, ili iweze kupata nyasi mwaka jana zaidi ya ng'ombe 7000 walikufa," anasimulia.

Anasema, mkaa wao unachomwa na kusafirishwa kuelekea maeneo ya mjini pasipo kufuatwa taratibu za kisheria, kwa sababu kinachofanyika wachoma mkaa huvamia usiku na kukata miti

"Wanatuharibia mazingira na mwisho wa siku miti itaisha, tunajikuta tunapata hasara. Tunashauri (serikali) wasishawishi watu kuja kukata miti.

"Wajitahidi kuangalia miundombinu mingine kwa ajili ya kupikia, ili misitu ibaki kuwa salama na jamii nyingine iweze kufurahia uwepo wa misitu," anasema.

Samweli anasema, wao wanajitahidi kutunza mazingira wanapowabaini wahalifu, huwakamata na kuwakataza wasiendelee kufanya uharibifu, licha ya kuendelea kukata miti.

"Tulikuwa na mabwawa ya asili na uoto wa asili, baada ya uharibifu huo wa ukataji wa miti mabwawa yamekauka, hakuna kitu kwa sasa. Tuna changamoto, tumehamisha mifugo kwenda maeneo mengine kama Mkuranga kutafuta malisho," anaeleza.

Samweli anaeleza kwamba kijiji hicho kina mifugo kati ya 20,000 hadi 25,000, nusu yao ipo nje ya kijiji, kutokana na ukataji miti ovyo.

Anasema, mtu anapohamisha mifugo kwenda maeneo mengine, anakutana na athari nyingi, ikiwemo kupata magonjwa na wakati mwingine mifugo kufa.

"Unaweza kusema unaokoa mifugo kwenda kupata malisho, baadaye ukajikuta unapoteza asilimia kubwa ya mifugo. Unaweza kuondoka na ng'ombe 300 ukarudi na 150. Hii ilitutokea mwaka jana katika kutafuta chakula cha mifugo yetu,"anasema.

"Mimi nilikwenda eneo la Mkuranga kupeleka mifugo yangu ili ikapate chakula, siku niliyoirudisha niligundua nimerudi na magonjwa, ng'ombe walikufa wengi," anaeleza.

Mkazi mwingine, Lengayo Koletu, anasema ukataji miti katika pori hilo umewaathiri sana katika kipindi cha nyuma, hali iliyosababisha kuwapo ukame katika eneo hilo.

Anaeleza wanaofanya uhalifu huo wamekuwa wakikaripiwa tu na hakuna hatua kama vile kutozwa faini, hivyo huondoka na kurudi wakiwa wamewasababishia uharibifu.

Koletu anasema wao katika nafasi yao wachungaji, wanajihisi vibaya, hawapendezwi na hali hiyo na kuna wakati wanapowakuta porini, huwafukuza ili kuhakikisha mazingira yanalindwa.

"Wanatukwepa, yaani wakituona, hao wanaokata miti kwa ajili ya kutengeneza mkaa wanatukimbia na sisi ni adui wao, hatukubali uharibifu wa mazingira wametusababishia jangwa mifugo haipati chakula," anasema.

**MWENYEKITI WA KIJIJI**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mbala, Lepa Mumbi, anasema tatizo hilo la ukataji miti kwa ajili ya mkaa unaosafirishwa kwenda maeneo ya mjini, imekuwa kero kwa sababu wanakosa vivuli vya mifugo ya kupumzika na hata kukosa nyasi.

Anasema makapi yanayobaki yanasababisha athari kwa mifugo, licha ya kupangiwa eneo hilo tangu mwaka 1975, miba inawachoma kwenye kwato na imekuwa kawaida, kwa siku wastani kati ya ng'ombe watano na sita, wanarudi wanachechemea.

"Pori zima linakuwa na miba na tatizo ni huo ukataji wa miti katika kijiji tunashindwa kuwakamata kuna wakati wanakuja kukata miti usiku wakijua huo muda tumelala,"anasema.

Anasema ni kawaida mara nyingi wamekuwa na kikao cha kitongoji na kuwaeleza marufuku inayowakabili kukata miti ndani ya eneo, ila wakaidi wanakata kwa kificho.

Mumbi anasema, hadi sasa kitongoji chao kimeathirika kwa asilimia 60 kuanzia mwaka 2018 kutokana na ukataji wa miti, sasa akiwa na ushauri, wizara husika ichukue hatua ikiwamo kuwa na katazo mahususi, kwa ajili ya kuthibiti uzalishaji mkaa, lengo ni kulinda rasilimali miti inayokatwa kienyeji.

**WAZALISHAJI MKAA**

Miongoni mwa wanaojishughulisha na ukataji miti katika kijiji hicho, Kondo Mwaule, anasema sasa wanafumbiwa macho, kutokana na hali zao mbaya za maisha ingawa ni kweli wanafanya uharibifu wa mazingira.

Anasema kwenye uhalifu huo, yupo kama wanavyofanya wengine na hapendi kufanya dhambi hiyo ya kukata miti na nchi kuiacha katika jangwa jambo analosema halipendezi.

"Serikali iangalie ifanye jambo gani ili tupate kula na wengine wasiingie katika ukataji miti, ikishindikana ujue wananchi wengi wataathirika,"anasema.

Julius Marwa, ni miongoni mwa wanaosafirisha mkaa huo kwa njia ya bodaboda, anajitetea wao hufuata sheria zote zinazotakiwa, ikiwemo kulipa ushuru, hivyo hawajui kama miti hiyo inakatwa kinyume cha utaratibu.

Anasema, changamoto waliyo nayo kwa kuwa hufungasha magunia matatu katika bodaboda moja, usalama wa afya zao unakuwa hatarini.

"Kwa upande wangu nimenusurika ajali nyingi na mabasi makubwa na hayo malori tunayopishana nayo barabarani. Hii kazi tunaifanya katika mazingira magumu, nashindwa kuicha kwa vile sina njia nyingine ya kunipatia kipato, wapo ndugu zangu niliowapoteza kwa ajili ya kazi hii," anasema.

AFYA

WAPANDAJI BODABODA JIFUNZENI...

# Ufahamu mgongo wako ulivyo, pingili zake na kinachotokea vinapojeruhiwa

Na Mary Geofrey

MAUMIVU ya mgongo ni tatizo linalowapata watu wengi kulingana na majukumu ya kazi zao, ikiwamo ya kusimama muda mrefu.

Katika kipindi chote cha maisha ya mwanadamu inatajwa kuna asilimia kubwa ya wanaoathiriwa na tatizo hilo, kwa mujibu wa takwimu za madaktari na zisizo rasmi waliloongea na Nipashe.

Wataalamu wanafafanua, maumivu hayo yanaweza kuwa ya kawaida, mengine yanayodumu kwa muda mrefu au yanaweza kuwa maumivu makali ya ghafla.

**DALILI ZAKE**

Wataalamu wa afya wanasema, maumivu ya mgongo si ya ugonjwa tu, bali ni dalili ya kuwapo ugonjwa au tatizo fulani mwilini na yanaweza kuwapo yenyewe au pamoja na dalili nyingine ya ghafla, muda mrefu, mfupi au sugu.

Kuna maumivu anayopata mtu ghafla baada ya kupata athari kama vile kuanguka anapopanda ngazi, uwanjani akicheza mpira au akinyanyua kitu kizito sana ndio maumivu ya muda mfupi yanatokea.

Ajali ya magonjwa au uvimbe, mara nyingi huwa ni chanzo cha maumivu sugu ya mgongo. Katika hilo, bingwa wa tiba ya mifupa kutoka Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), Dk. Tumaini Minja, anafafanua kuwa mwili wa binadamu umejengwa na misuli inayojishikiza kwenye mifupa.

Misuli hiyo anaitaja inakazwa na kulegea, ikizalisha nguvu inayoufanya mwili wa binadamu utembee na kushughulisha maungo hayo kila mara.

Hivyo, eneo la mgongo lote hadi kwenye nyonga ni muunganiko wa misuli, ambayo imejishikiza katika maeneo tofauti, ikiwamo mifupa ya uti wa mgongo ambayo imezoeleka kuitwa pingili za mgongo.

Inatajwa, baina ya pingili moja na nyingine, kuna 'tishu' duara ambazo ni mithili ya mpira unaozunguka kimiminika, mtaalamu Dk. Minja akifafanua:

"Hizo huitwa diski za uti wa mgongo. Kazi yake kubwa ni kupunguza mkazo na mgandamizo baina ya pingili moja na nyingine."

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, hizo pingili huwa zinachakaa kuendana na umri, pia mabadiliko ya kimwili, hivyo ufanisi wa kazi yake hupungua.



Mandhari ya ajali za pikipiki, ambazo zimekuwa na athari kubwa kwa abiria na waendeshaji, ikiwamo mgongoni. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**MGONGO ULIVYOGAWANYIKA**

Mgongo kitaalamu unaelezwa kugawanyika katika sehemu ya shingo (cervical), kifua (thoracic), kati na kiuno (lumbar) na mkia (sacral and coccygeal).

Dk, Minja anasema, sehemu ya chini ambayo ni kiuno, pingili zake pamoja na diski ziko pana na hiyo ni kwa sababu zinabeba uzito mkubwa katika eneo hilo.

Pia, anaeleza kwamba, mgongo ulivyo haujanyooka, bali una mikunjo ambayo ina maumbile ya utendaji ambayo kitaalamu yanatajwa 'baiomekaniki' yanasaidia kusawazisha na kuleta uwiano wa mgandamizo kutoka kichwani hadi chini na ile kutoka chini kurudi juu (ground reaction forces).

Namna ya uwiano wa mgongo, unaelezwa pia huathiriwa na kiuno na nyonga, kwani ukaaji mbaya eneo la nyonga, unachangia mabadiliko yanayoenda moja kwa moja hadi kwenye mgongo.

"Mtu akikaa vibaya kwenye nyonga, basi mabadiliko huja kumfikia mpaka kwenye mgongo," anaeleza Daktari Minja.

**KUVUNJIKA PINGILI**

Daktari huyo bingwa, anasema kuvunjika pingili za mgongo zinahusisha pingili za mgongo na uti wa mgongo na kimoja kinapopata shida au vyote, huleta athari kubwa kimaumbile.

Anasema, mambo yanayosababisha kuvunjika pingili za mgongo, inajumuisha ajali kama za magari barabarani, pikipiki au wajenzi na wakwezi wanapoanguka.

Anataja sababu nyinginezo, ni watu wanaodhurika na silaha za moto kama vile risasi zinazosababisha kuvunjika pingili za mgongo. Pia, wapo wanaoumia michezoni hata kusababisha kuvunjika pingili hizo za mgongo.

**KAZI ZA MIFUMO**

Dk. Minja anasema, kazi inayofanywa na mfumo wa pingili za mgongo ni kupitisha mishipa ya fahamu inayofikisha fahamu kwenye mikono, kupumua, kuchakata chakula tumboni, kutoa nguvu ya kunyanyuka, kutembea na kukunja miguu.

Anasema, ili kujua kama umevunjika pingili za mgongo ni kusikia maumivu katika eneo ambalo mvunjiko umetokea na mifupa ya pingili za mgongo imeanzia shingoni hadi kiunoni.

Hapo anafafanua kwamba, kwa kawaida anayepata madhara hupata uvimbe katika eneo husika la mgongo na mgonjwa anaweza kuanza kusikia hali ya kukosa fahamu, pia akipoteza nguvu za mikono au miguu.

Dk. Minja anasema hiyo inatokana na hali ya upitishaji mishipa ya fahamu kwenda sehemu mbalimbali za mwili hadi kifuani, inakuwa ngumu, hata mhusika anashindwa kupumua.

Anaeleza, mgonjwa anaweza kutokwa na haja bila kujitambua, ikiwamo hilo la kushindwa kuzuia haja kubwa na ndogo.

**MADHARA YAKE**

Dk. Minja anasema, mtu anapovunjika uti wa mgongo, mgonjwa anaweza kupooza miguu au mikono, kutegemea na sehemu aliyoumia ya juu au chini.

Anataja madhara mengine, ni mgonjwa kushindwa kuzuia haja zote kwa sababu anakuwa hasikii kitu na wala mishipa ya fahamu haifanyi kazi, hata wapo wanaopata ulemavu wa kudumu, wakiwa wamepoteza uwezo wa kufanya kitu chochote kile.

Lingine kwa mujibu wa Dk. Minja ni mgonjwa huyo anapolala muda mrefu kwa sababu ya tatizo hilo, anaweza kupata vidonda mwilini na kuzua tatizo jipya , akifafanua ni tatizo linalochukua sura zaidi kati ya 18 hadi 45.

**MATIBABU NA KINGA**

Mtaalam huyo anafafanua matibabu yake, yanajumuisha kutumia dawa za kumeza au sindano, upasuaji na mazoezi tiba (physiotherapy).

Anasema, upasuaji hufanyika kwa wenye matatizo makubwa, ili kurejesha hali ya zamani ya pingili iliyopata shida.

Dk. Minja anaushauri umma kuepuka kupata tatizo la kuvunjika pingili za mgongo, kwa kuwa makini dhidi ya ajali na hasa za barabarani.

Pia, anawataka Watanzania wanaofanya kazi katika maeneo hatarishi na wale wanamichezo kuwa makini dhidi ya majeruhi wanapokuwa wakitekeleza majukumu yao.



AFYA

KAMPENI ELIMU AFYA YA MTOTO...

# Ijue Programu ya Sayansi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo kwa Mtoto

## •Waziri Dk. Gwajima atabiri mafanikio yaja




Waziri Gwajima akiwa na kitabu chenye mwongozo wa Programu ya Sayansi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Sabato Kasika**

HADI sasa kitaifa na kimataifa kuna jicho la kipekee kwamba suala la malezi bora ya watoto linapewa umuhimu wa kimataifa, katika namna mbalimbali.

Kiserikali, nchini hadi sasa kuna programu maalumu ambayo maudhui yake ni Mafunzo ya Kitaifa ya Sayansi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto tangu kuzaliwa, hadi anapofika umri miaka minane, ikipitishwa kwa kada mbalimbali.

Miongoni mwa wanaoelimishwa ni maofisa ustawi na maendeleo ya jamii na wadau wengine kutoka asasi za kiraia, ambako kunaelezwa ni mwanzo wa kuzifikia kada nyinginezo, ikiaminika kupitia njia hiyo, jamii inaweza kupata uelewa sahihi.

Katika hilo, inaelezwa kuna aina ya hatua inayoelimisha namna ya kuwapa watoto, ikiwa pia ndio nyenzo ya kumaliza vitendo vya ukatili kwa watoto.

Jamii hadi sasa inapewa wajibu wa kuzingatia malezi na makuzi katika kupambana na vitendo vya ukatili kwa watoto na watu wengine, hivyo kuifanya iwe na mwamko wa kupambana na mambo hayo.

Mustakabali wa malezi na makuzi mazuri kwa watoto, msingi wake unatajwa kugusa lishe bora, ambayo ni muhimu kwa afya zao, wazazi, walezi na jamii.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dk. Dorothy Gwajima, anafafanua hayo katika ufunguzi wa mafunzo ya siku sita jijini Dodoma wiki hii, akiwahimiza wanahabari kuelimisha umma.

Rai yake ni kwamba, waandishi wa habari wakitumia vyema kalamu zao wanaweza kuinua taaluma zao kuelimisha kwenye programu ya Sayansi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, kuhusu umuhimu wa malezi bora ndani ya kipindi cha umri uliotajwa.

**PROGRAMU INAKOELEKEA**

Waziri Gwajima anafafanua mafunzo hayo ya Sayansi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto yanalenga kuimarisha utekelezaji Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto iliyozinduliwa Desemba, 2021 ili kutekeleza na kuleta matokeo chanya kwa taifa.

Anaongeza kuwa, programu hiyo ni kielelezo cha Rais kujielekeza kuweka misingi imara ya malezi na makuzi ya watoto wa taifa, ili waendelee kuwa na fursa ya kukuza vipaji vyao tangu hatua za awali, hivyo kuwa na fursa pana ya kufika mbali katika utoaji mchango kitaifa.

"Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (TECDEN), shirika la Children in Crossfire na Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania kupitia mradi mnaoutekeleza unaoitwa 'Mtoto Kwanza' kwa kutuwezesha kukutana hapa, ili kupata mafunzo ya Sayansi ya Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto," anasema Dk. Gwajima.

Anafafanua kuwa serikali inatambua mafunzo hayo ni fursa ya kipekee kuwajengea uwezo kundi kubwa la wataalamu watakaokuwa wajuzi kuhusu utekelezaji Programu Jumuishi ya Kitaifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, kuchochea uwekezaji malezi na makuzi bora ya watoto nchini.

Dk. Gwajima, ambaye kitaaluma ni tabibu, anaeleza:" Tutakuwa na wataalamu wengi kwenye maeneo mbalimbali, hivyo kuwa na uhakika kuwa programu hii inaratibiwa na kusimamiwa na watu sahihi wenye uelewa kwenye malezi na makuzi ya watoto."

**KUTOKA WIZARANI**

Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Sebastian Kitiku, anasema elimu kwa kada hizo ni mwanzo wa kuzifikia kada nyinginezo, ili ziwe karibu na kuhakikisha jamii inakuwa na uelewe wa namna ya kuwapa watoto malezi bora kupitia programu hiyo.

"Elimu hii ambayo inatolewa kwa muda wa siku sita, ni mwanzo tu, lakini lengo letu ni kuwafikia watu wa kada zote nchini kwa kuwatumia maofisa ustawi na maendeleo walipata elimu hii," anafafanua Kitiku. ambaye pia ni Mkurugenzi wa Watoto.

Anasema, maofisa ustawi na maendeleo ya jamii, watakuwa na kazi ya kwenda kwenye vituo vyao vya kazi nchi nzima kuweka mipango ya kuifikia jamii na kuipa elimu hiyo muhimu.

Mkurugenzi Mkazi wa taasisi ya Crossfire, Craig Ferla, anasema mwelekeo ulioko ni kuandaa kadi ya kujipima kwa kila mmoja, ili kuona kama washiriki wanapiga hatua kwa elimu inayotolewa na lengo lililokusudiwa.

"Mheshimiwa waziri utakumbuka kuwa ulipomwakilisha mheshimiwa Rais, wakati wa uzinduzi wa programu hii, uliagiza suala la Score Card. Leo tunaomba tukuhakikishie kuwa suala hilo tumelizingatia, hivyo katika utendaji wetu tumeona tuwe nalo," anasema Craig.

Washiriki kutoka Tanzania Bara na Visiwani wakiwamo maofisa waandamizi wa serikali kuu, mikoa na kutoka asasi za kiraia wakiwamo waandishi wa habari kutoka klabu za waandishi wa habari, wanapata mafunzo hayo.

**VIKWAZO VYA MALEZI**

Waziri Dk. Gwajima anasema, kumekuwapo vitendo vya ukatili kwa watoto, chanzo chake kikiwa malezi duni na anawataka kufichua viashiria vya vitendo hivyo vinavyotokea nyumbani na hata shuleni.

Ni kauli yake katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika,mwezi uliopita akiwasisitiza wasiogope, badala yake waonapo vitendo au viashiria, watoe taarifa kwa watu wanaowaamini na dawati la jinsia vituo vya polisi.

"Wanangu! Baba akikufanyia ukatili, mwambie mama na kama ni mama, basi mwambie baba au kama unaona huwezi kuwaambia wote, basi mwambie mtu unayemwamini," anasema.

Akitoa takwimu za matukio ya ukatili kwa watoto katika kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka jana, anasema matukio yaliyoripotiwa Polisi ni 11,499 ikilinganishwa na matukio 15,870 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na kupungua matukio 4,371 ikiwa ni asilimia 27.5.

"Mikoa iliyoongoza ni Arusha (808), Tanga (691), Shinyanga (505), Mwanza (500) na Mkoa wa Kipolisi Ilala (489). Makosa mengi yakiwa ni ubakaji (5,899), mimba za wanafunzi (1,677) na ulawiti (1,114)," anasema.



Watoto wakiwa kweye mjumuiko wa michezo yao. **PICHA: MAKTABA.**





## RC abuni utaratibu utoaji mikopo kwa wananchi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, imebuni utaratibu wa kuanza kutoa mikopo kwa wananchi watakaowasilisha mawazo ya kibiashara ili kujikwamua kiuchumi.

Fedha zinazokopeshwa zinatokana na fungu kusaidia jamii ambalo hutolewa kila mwaka na serikali na mkoa hupewa Sh. milioni 20 huku kila wilaya akipata shilingi milioni tano.

Mkuu wa Mkoa huo, Anthony Mtaka, alibainisha hayo juzi kwenye hafla ya utoaji wa mikopo kwa baadhi ya wakazi wa Dodoma waliofika ofisini kwake kuomba misaada.

Alisema fedha hizo zitatolewa kwa riba ya asilimia mbili na utaratibu huo utafanyika kwa mwaka mmoja na baadaye kufanya tathmini ili kuangalia kama una mafanikio.

"Tumeanza kwa fedha tunazopewa Sh. milioni 20, tuwape nafasi vijana na wananchi wa Mkoa wa Dodoma wenye mawazo ya kibiashara yatakayoanzia Sh. 50,000 hadi Shilingi milioni tatu, Ofisi ya Mkoa ya Biashara na Uchumi, itapitia mawazo husika na kuwapatia hizo fedha kwenye akaunti," alisema.

Alisema iwapo utaratibu huo utakuwa na mafanikio, utachochea taasisi za fedha kusaidia mpango huo na kila mwaka wananchi watatangaziwa kuomba mikopo.

Mtaka alisema kwasasa wametoa mikopo ya Sh. milioni 13 kwa wananchi ambao walifika kwenye ofisi hiyo wakiomba msaada na kuwasilisha mawazo yao.

"Sisi mkoa tunataka tusaidie wazo lako la biashara lililopo kichwani, mimi sina uhakika wa kula na nikiamka sijui nafanya shughuli gani, tunataka wazo kwamba nikipata kilo 100 za biashara ya mchele naweza kuishi."

"Utatuambia mimi nitachukua kilo moja kwa Sh. 1,800 mimi nitauza Sh. 2,200, sisi tutakupa kilo 100 na kuzibeba hadi nyumbani Sh. 10,000, kubeba hadi sokoni Sh. 10,000 jumla Sh. 200,000 ukiuza hapa unapata Sh. 20,000 faida yako, na ukizungusha una uwezo wa kupata uhakika wa kula hivyo unatoka sasa kwenye hali ya kukaa bila kazi," alisema.

Alisema kila aliyefika katika ofisi hiyo kwa lengo hilo amepewa fedha kulingana na wazo lake ambalo ameliweka kimaandishi na limepitiwa na ofisi hiyo.

"Leo tunatoa fedha kwa watu 16 ambao mawazo yao jumla ni Sh. milioni 13, kuna mtu ameomba kuuza dagaa tumempa Shilingi milioni moja, kuna mtu ameomba duka la rejareja tumempa hela, lakini tumeweka riba ya asilimia mbili," alisema.

Mmoja wa wanufaika wa utaratibu huo, Mkazi wa Kizota, Nyundo Bura, alisema alipata ajali ya pikipiki mwaka 2020 ilimfanya akatwe mguu na kumlazimu kushindwa kufanya kazi za kulima alizokuwa akizifanya awali, ameomba mkopo wa Shilingi milioni moja ili kufanya biashara ya vyakula.

Naye Jacquline Msuya, alisema kutokana na kufukuzwa na mume wake ilimlazimu kwenda kuomba msaada kwenye ofisi hiyo na kutakiwa kuandika andiko la kuuza keki na vitafunwa na amepatiwa mkopo wa shilingi milioni moja.



Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu, akizungumza na mashekhe, maimamu, walimu na waumini wa dini ya kiislamu, wakati wa shindano la kusoma Qur'an tukufu, lililoandaliwa na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Wilaya ya Dodoma, kwenye viwanja vya msikiti wa Mukadam Chang'ombe juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TOSCI yabaini uuzaji mbegu zilizoisha muda

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

TAASISI ya Udhibiti wa Mbegu Tanzania (TOSCI), imebaini kuwapo na kasoro nyingi kwa wafanyabiashara wa mbegu ikiwamo kuuza zilizoisha muda na inayodhoofisha mtiririko na mnyororo wa thamani.

Kutokana na hali hiyo, TOSCI inatekeleza mpango madhubuti unaolenga kuwasaidia wafanyabiashara wa mbegu nchini kuendesha biashara zao kwa kuzingatia Sheria ya Mbegu ya Mwaka 2003 na kanuni zake.Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, Dk. Patrick Ngwediagi, alisema baadhi ya wafanyabiashara wanauza mbegu zilizoisha muda huku wengine wakikosa uaminifu kwa kufungua vifurushi vya mbegu ili kuzipima na kuziuza kwa viwango tofauti tofauti.

Alitaja kasoro nyingine ni baadhi ya wafanyabiashara wa mbegu hawatambuliki wala hawajajiandikisha TOSCI, jambo ambalo ni kinyume na sheria hiyo na kanuni za mbegu za 2007.

"Baada ya kuchunguza na kugundua dosari zilizotajwa katika uuzaji wa mbegu, tumeamua kwa uzalendo kuchukua hatua ya kuwaelimisha wafanyabiashara wa mbegu ili kuwasaidia kufanya biashara zao kwa kuzingatia sheria na katika viwango vinavyohitajika," alisema.

Aliongeza kuwa baadhi ya wafanyabiashara wa mbegu wanauza bila kuwa na nembo rasmi za TOSCI au Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD).

"Kulingana na kanuni husika, mbegu zote zinazozalishwa nchini zinatakiwa kuwa na label rasmi kutoka TOSCI, ambapo zile zinazotoka nje ya nchi lazima ziwe na lebo ya OECD," alifafanua.

Alisema mpango huo pia unalenga kuwajengea uwezo wafanyabiashara hao njia za kitaalamu za kuhifadhi mbegu, huku akibaini kuwa baadhi ya wafanyabiashara walikuwa wakihifadhi sakafuni na wengine wakihifadhi pamoja na mbolea jambo ambalo si sahihi kitaalamu.

Alisisitiza kuwa TOSCI haitasita kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya wafanyabiashara wote ambao watabainika kuuza mbegu bila kuzingatia sheria.

"Kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Mbegu ya mwaka 2003, mtu/mfanyabiashara yeyote atakayebainika kukiuka kanuni zilizowekwa atatozwa faini ya kuanzia Shilingi milioni moja hadi milioni 500, au kifungo cha mwaka mmoja jela," alisema.

Alisema taasisi hiyo ina mipango mingi ya kutekeleza katika kuhakikisha nchi inapata aina bora za mbegu.

## Chongolo aweka jiwe la msingi majengo nane ya biashara

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameweka jiwe la msingi la mradi wa majengo nane ya biashara pembezoni mwa Uwanja wa Jamhuri jijini hapo utakaogharimu zaidi ya Sh. milioni 991 huku akiagiza ngazi zote za chama kubuni miradi na kujiimarisha kiuchumi.

Mradi huo utakaokuwa na vyumba vya biashara 172 unatekelezwa na CCM Mkoa wa Dodoma na unatarajiwa kuwezesha kukusanywa zaidi ya Shilingi bilioni moja kwa mwaka.

Akizungumza jana alipokuwa akiweka jiwe hilo, Chongolo alisema mradi huo ni mkubwa na ni mfano wa kuigwa kwa ngazi zingine za chama ili kujiendesha kwa kujitegemea badala ya kutegemea hisani.

"Nipongeze uongozi wa Mkoa wa Dodoma wa CCM kwa kuona umuhimu wa kujielekeza katika kujiimarisha kiuchumi, na kasi ya ujenzi ni nzuri ndani ya miezi mitatu naona ujenzi upo zaidi ya asilimia 95, hatua hii itasaidia kusukuma gurudumu la kujikwamua na kujiendesha kwa kujitegemea badala ya kusubiri hisani, siasa ni uchumi bila uchumi siasa haiwezi kuwa imara," alisema.

Awali, akisoma taarifa ya mradi huo, Katibu wa CCM Mkoa wa Dodoma, Pili Agustino, alisema Aprili 5, mwaka huu Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa huo ilipitisha ujenzi wa majengo hayo yenye vyumba 172.

"Mradi huo ulianza Aprili 11, mwaka huu na hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 95, yapo katika hatua ya umalizaji, huu unatekelezwa kupitia ujenzi shirikishi isipokuwa gharama za ujenzi wa msingi zilitumika fedha za mapato ya ndani ya chama Sh. milioni 123.2 awali makadirio ilikuwa Sh. milioni 187.9 na yalikuwa ni makubaliano ya chama na wapangaji wa vyumba hivyo," alisema.

Alisema vifaa vyote vya ujenzi vipo eneo la mradi na awali ilipangwa kugharimu Sh. milioni 891, lakini kutokana na kupanda kwa gharama za ujenzi, mradi kwa sasa utagharimu zaidi ya Sh. milioni 991.

"Katika mradi huu kuna vyumba ambavyo gharama ya kupanga ni Sh. 500,000 na makusanyo ni Sh. milioni 300 kwa mwaka, kwa jumla matarajio ya mradi ni kukusanya mapato ya Sh. bilioni 1.089, kupitia mradi huu tumepanga kusaidia wilaya ambazo hazina miradi," alisema.

Katibu huyo alisema hadi sasa wamepanga kuongeza nguvu kwa Wilaya ya Kongwa inayojenga ukumbi, Wilaya ya Bahi wanajenga ofisi na vyumba vya biashara, Wilaya ya Chemba watajenga mgahawa mkubwa wa kisasa.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ni Mwenyekiti wa chama hicho Taifa, kupitia vikao anavyoongoza kwa kuagiza kuboresha miradi iliyopo na kuanzisha mipya na kwa Dodoma wanatekeleza maelekezo hayo kwa vitendo.





# Serikali kujenga miradi 13 ya kilimo cha umwagiliaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, inakusudia kujenga miradi 13 ya umwagiliaji mkoani hapo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua.

Mtendaji Mkuu wa Tume ya Umwagiliaji nchini, Raymond Mndolwa, aliyasema hayo jana jijini hapo, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu ziara yake katika mikoa ya Katavi, Rukwa, Songwe na Mbeya kuwa miradi hiyo itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Alisema kati ya miradi hiyo, 11 ipo katika Wilaya ya Mbarali, mmoja katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela na mmoja katika Halmashauri ya Busokelo, wilayani Rungwe.

Mdolwa alisema lengo la serikali ni kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua pekee kwa maelezo kuwa kilimo cha aina hiyo tija yake huwa ni ndogo inapotokea matatizo ya hali ya hewa.

Alisema miradi hiyo itakuwa ya ujenzi wa skimu za umwagiliaji pamoja na kukarabati za zamani ambazo zimechakaa ili kuongeza ufanisi wa uzalishaji wa mazao.

Aliitaja miradi hiyo kuwa ni wa Makwale katika Wilaya ya Kyela wenye ukubwa wa hekta 2,500 na Skimu ya Mbaka iliyoko katika Halmashauri ya Busokelo, wilayani Rungwe wenye ukubwa wa hekta 300.

Vilevile, aliitaja miradi iliyopo wilayani Mbarali kuwa ni wa Lwanyo wenye ukubwa wa hekta 1,000, Gonakuvagogolo (250), Matebete (1,200), Chosi (1,700), Helman (400), Uturo (2000), Isenyela (1,000) na Makangarawe (1,100).

Miradi mingine ni Skimu ya Madibira yenye ukubwa wa hekta 3,200, Mbuyuni-Kimani (3,000) na Msesule (4,500) na kati ya hizo, 1,500 zitajengwa katika mwaka wa fedha 2022/2023.

"Pia kwenye ziara hii tumekagua skimu za Igumbilo/Isitu na Njombe zote za wilayani Mbarali zenye jumla ya hekta 900 na tumezikagua ili ziwekwe katika mipango ya usanifu na ujenzi," alisema Mndolwa.

Serikali pia inakusudia kuanza kujenga mabwawa ya kuvunia maji ya mvua ili kuimarisha zaidi kilimo cha umwagiliaji.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema serikali ya mkoa huo itahakikisha inatoa ushirikiano kwa tume hiyo ili miradi yote ikamilike na kuwanufaisha wakulima wa mkoa huo kwa kuwaongezea kipato na uhakika wa chakula.

Homera alisema kwa msimu uliopita wa kilimo, uzalishaji wa mazao mbalimbali ulipungua kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yalisababisha kupungua kwa mvua.

"Hatuwezi kukuza sekta ya kilimo kwa kutegemea mvua pekee, kwa hiyo naipongeza sana tume ya umwagiliaji kwa kufanya ziara hii katika mkoa wetu na tuna uhakika hii itatusaidia sana kuongeza uzalishaji," alisema Homera.

Aliwataka wakulima wa mkoa huo kujipanga kwa ajili ya kuzitumia vyema skimu hizo zitakapokamilika ili kuongeza uzalishaji na kuwa na uhakika wa chakula na kipato.



Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano cha Vodacom Group, Mwamvita Makamba (katikati), akichangia mada ya mageuzi ya kimkakati ya afya nchini kupitia muungano wa biashara ya afya, wakati wa kongamano la pili la Mkapa Legacy 2022, mjini Zanzibar jana, ambapo Vodacom Tanzania Plc wanatoa huduma ya afya kupitia programu ya M-mama pia ni mdhamini wa kongamano hilo. Kulia ni Sarah Maongezi kutoka Taasisi ya Agakhan Health Services na mwongoza mjadala, Dk. Faustine Ndugulile. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bilioni 41/- zatengwa utekelezaji miradi maji

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI imetenga zaidi ya Sh. bilioni 41 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo ya pembezoni mwa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya kwa lengo la kuwapunguzia wananchi tatizo la kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Mbunge wa Jimbo la Lupa, Masache Kasaka, alisema kumekuwapo na matatizo ya upatikanaji wa maji hususan katika maeneo ya vijijini kikiwamo kitongoji cha Itumbi, Kata ya Chalangwa wilayani humo na tayari imeanza kutafutiwa ufumbuzi.

Kasaka alisema licha ya kuwapo kwa miradi ya kimkakati, pia kuna wadau wanaounga mkono juhudi za serikali kuhakikisha wananchi wanapata maji kwa kuchimba visima virefu vya maji wakati utekelezaji wa miradi mikubwa ukiendelea.

"Tatizo la maji ni kubwa sana, lakini tangu nimeingia kuwa mbunge nimepambana kwa hali na mali, Wizara ya Maji, imesogeza huduma ya majisafi kwa kuelekeza miradi mikubwa hususan katika mji wa Makongorosi," alisema Kasaka.

Alisema anawasilisha kero ya maji serikalini ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma kwa wakati ili watekeleze majukumu yao ya uzalishaji badala ya kutumia muda mrefu kuitafuta huduma hiyo.

Alisema pia amekuwa akiwasilisha kero mbalimbali za wananchi serikalini ili zitafutiwe ufumbuzi na hivi karibuni alilalamikia ukosefu wa soko la uhakika la tumbaku na tayari ufumbuzi umepatikana kwa serikali kupeleka kampuni mpya.

# Shirika launda kamati maalum kusaka watoto wenye ulemavu waliofichwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKA lisilokuwa la kiserikali la Child Support Tanzania (CST) limeunda kamati maalumu ya kuwasaka na kuwafichua watoto wenye ulemavu wanaofichwa majumbani ili wapatiwe haki zao za msingi kama watoto wengine.

Akizungumza katika kikao cha kamati hiyo juzi, Mratibu wa miradi wa kuibua watoto hao, Hildergard Mehlab, alisema CST pekee haiwezi kufikia azma ya kuwapeleka watoto wenye ulemavu shuleni bila kushirikiana na wadau wengine.

Alisema jamii haina uelewa wa kutosha kuhusu kundi hilo na ndiyo maana wengi wa watoto hao hufichwa majumbani na kukosa haki zao za msingi ikiwamo elimu.

Mradi huo wa miaka mitatu una lengo ni kuongeza watoto wenye ulemavu katika vituo vya elimu jumuishi, kuhamasisha jamii kuwapeleka watoto shule na upatikanaji wa ubora wa elimu inayotolewa shuleni. Alisema mradi huo utalenga kufanya tathmini ya ufunzaji bora kwa watoto wenye ulemavu, utafiti wa watoto wenye ulemavu ili kujua aina ya tatizo alilonalo kwa ajili ya kumpatia matibabu na visaidizi na kujua mahali sahihi anapopaswa kupata hiyo elimu.

Aliongeza kuwa lengo la kamati hiyo itakayohudumu hadi 2024 itakuwa na kazi ya kulisaidia Shirika la CST kuhusu upimaji na uwekwaji wa mahala sahihi pa kupata elimu jumuishi, kufuatilia ubora wa elimu, kushirikisha jamii na wadau utoaji huduma kwa watoto wenye ulemavu pamoja na kuongeza ushiriki na uhusiano baina ya shirika na serikali.

Mratibu huyo alisema majukumu mengine ni pamoja na kulisaidia shirika kuongeza uwezo wa kutathmini na ufuatiliaji wa huduma kwa watoto wenye ulemavu, kuongeza uwezo wa shule ya CST ili iweze kuongeza usajili wa watoto katika kituo cha utoaji wa elimu jumuishi.

"Mradi huu utalenga shule maalum katika Mkoa wa Mbeya ambapo gari maalumu litanunuliwa ili kurahisisha wajumbe kufika katika maeneo mbalimbali wakati wa kuhamasisha jamii kuwafichua watoto wenye ulemavu majumbani," alisema Mehlab.

Alizitaja shule zitakazonufaika na mradi huo kuwa ni Mwenge na CST zilizoko katika Jiji la Mbeya, Chimala na Madibila, Wilaya ya Mbarali, Mpandapanda na Katumba Wilaya ya Rungwe, Kyela na Mwenge, Wilaya ya Kyela, Lupata na Kandete Halmashauri ya Busokelo, Makongolosi na Kibaoni Wilaya ya Chunya na Nsongwe juu kutoka Wilaya ya Mbeya.

Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo, waliipongeza taasisi hiyo kwa kubuni mradi huo kwa kuwa kwenye jamii uelewa ni mdogo kuhusu watoto wenye ulemavu na wenye mahitaji maalumu.

Mmoja wa wajumbe hao, Damas Mwambeje, kutoka Chama cha Walemavu Jiji la Mbeya, alisema mradi huo utasaidia kuongeza idadi kubwa ya watoto kwenda shule badala ya kufungiwa majumbani.

Alisema pamoja na jambo hilo kuanzishwa na CST ni vema elimu ikaendelea kutolewa kwa jamii kupitia mikutano, matamasha, vyombo vya habari na vipeperushi mbalimbali ili jamii ione umuhimu wa kuwapeleka watoto shule na baada ya muda mfupi wengi wao hubadilika tofauti na kukaa nao majumbani.





# Mkuya aipongeza Benki ya Dunia kuisaidia Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Salum Mkuya, ameipongeza Benki ya Dunia kwa kuisaidia Zanzibar katika nyanja mbalimbali ikiwamo ya kuwawezesha wanawake kiuchumi.

Aliyasema hayo jana kwa nyakati tofauti wakati uongozi wa benki hiyo ukiongozwa na Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia, Victoria Kwakwa, ulipotembelea miradi mbalimbali ya maendeleo inayofadhiliwa na benki hiyo ikiwamo kuwawezesha wanawake kiuchumi kupitia kilimo cha mwani huko Muungoni Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema benki hiyo pia inaisaidia Zanzibar katika miradi ya mageuzi ya miundombinu ya umeme ikiwamo uwekaji wa miundombinu ya uzalishaji umeme mbadala wa jua.

Alisema mradi huo unaofadhiliwa na Benki ya Dunia una thamani ya Dola za Kimarekani milioni 140 utasaidia katika uzalishaji wa umeme wa jua ambao ni mkombozi wa mazingira.

Alisema kwa mwaka 2022 hadi 2024, benki hiyo imetenga Dola bilioni 2.1 kwa Serikali ya Tanzania kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo na Zanzibar itaifaidika na miundombinu ya ujenzi wa mahakama, miundombinu ya kilimo na upatikanaji wa majisafi na salama.

"Benki ya Dunia inaisaidia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar, tunafaidika na kuna fedha tunazopata kutoka benki hiyo inayosaidia bajeti ya serikali na tunapata mgao wa asilimia 2.5 alisema," alisema Dk. Mkuya.

Alisema Benki ya Duani ni mshirikika mkubwa wa maendeleo Zanzibar na wanashirikiana katika kuimarisha sekta ya afya hasa kupunguza vifo vya wajawazito na watoto na miradi ya kuwawezesha wanawake kiuchumi.

Wakizungumza mbele ya Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia, wakulima wa mwani wa kijiji cha Muungoni, walisema kuwa licha ya kilimo hicho kuwa ni mkombozi wao katika kupata kipato, kina changamoto zake na kuhitaji kutatuliwa.

Mwenyekiti wa kikundi cha wakulima wa mwani (Tuko kweli), Riziki Ame Makame, alisema kuwa wanahitaji vifaa vya ukaushaji wa mwani ili kulipa thamani zao hilo.

Alisema bado bei ya mwani ya kilo moja 6,000 haikidhi mahitaji kutokana na ugumu wa kilimo hicho ambacho zaidi ya asilimia 90 kinalimwa na wanawake.

"Hatutaki tuishie kulima pekee, lakini tunahitaji kuutumia mwani kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali hivyo tunahitaji mashine kwa ajili ya kusarifu mwani," alisema.

Kwa upande wake, Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia, Victoria Kwakwa, aliwapongeza wakulima hao kwa kazi ngumu wanayofanya ya kilimo hicho bila ya kukata tamaa na kuahidi kuwa benki hiyo itawasaidia ili kukifanya kilimo hicho kuwa cha kisasa na kukuza biashara zao.

"Nimejionea hapa biashara mnazotengeneza zinazotokana na mwani ni nzuri na zenye ubora niwasihi mwendelee kuzalisha kupata kipato na kujikomboa kiuchumii," alisema Kwakwa.



Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia Kanda ya Kusini mwa Afrika, Victoria Kwakwa (wa tatu kulia), akipokea zawadi ya kitenga kutoka kwa mwenyekiti wa kikundi cha wajasiriamali cha Tuko Kweli cha kijiji cha Muungoni, Kusini Unguja, Riziki Ame Makame, wakati alipotembelea miradi inayofadhiliwa na benki hiyo, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Watendaji serikali watakiwa kuwa wafanisi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATENDAJI wa taasisi za serikali wametakiwa kuwajibika ipasavyo ili kuleta ufanisi mzuri wa kazi zao.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, aliyasema hayo katika kikao kazi kilichowakutanisha mawaziri na manaibu mawaziri wote wa serikali kilichofanyika ofisini kwake Vuga Zanzibar.

Hemed alisema, mawaziri ni wasimamizi wakubwa wa wizara zao na kwamba ni lazima kuwa na mshikamano na kuwasimamia watumishi walio chini ya wizara zao ili kuhakikisha wanawajibika ipasavyo katika kuleta maendeleo nchini.

Alisema kuwa ni lazima viongozi wakafanya kazi kwa bidii na kwa ushirikiano mkubwa ili kumsaidia Rais kutimiza azma ya serikali ya kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Aliwataka mawaziri kusimamia vyema ulipaji wa kodi za serikali katika wizara zao na kuwataka kutoa taarifa ya utekelezaji wa mipango kazi waliojiwekea kila baada ya miezi mitatu ambayo itajumuisha kiwango cha kodi kilichokusanywa ndani ya kipindi hicho.

Aliwataka mawaziri hao kushirikiana na kutoa taarifa kwa vyombo vya habari kwa kila baada ya muda ili kumpunguzia mrundikano wa maswali Rais wakati anapokutana na waandishi wa habari kila mwisho wa mwezi wakati asilimia kubwa ya majibu ya maswali hayo tayari yameshatekelezwa.

Pia, aliwataka mawaziri hao kuisimamia vyema miradi inayotekelezwa chini ya wizara zao ili ijengwe kwa kiwango kinachokubalika na iendane na thamani ya pesa zilizotumika.

Kwa upande wao mawaziri na manaibu waziri, waliahidi kuyafanyia kazi yote waliyoagizwa katika kikao hicho ili kuwatendea maendeleo wananchi.

# Makamu Othman amzungumzia Hayati Mkapa kiuchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othaman, amesema Hayati Benjamin Mkapa alifufua uchumi, sera thabiti za uchumi mkuu pamoja na mageuzi ya kimuundo na sera ya ubinafsishaji iliyoanzishwa na mtangulizi wake.

Alisema utawala wake ulipata misingi ya uchumi mkuu, ambayo iliongeza imani ya wawekezaji kwa nchi na serikali.

Aliyasema hayo jana wakati wa kongamano la kumbukizi ya Mwasisi wa Taasisi ya Mkapa (Mkapa Foundation) Benjamin Wiliam Mkapa, lililofanyika mjini hapo.

"Ni kutokana na juhudi hizo leo tunakusanyika hapa kufanya tafakari hizi na kuweka mikakati ya nafasi ya sekta binafsi katika kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia uwekezaji katika sekta ya afya," alisema Othman.

Alisema Hayati Mkapa, alichukua jukumu muhimu katika kuimarisha taasisi za uwajibikaji, kubadilisha sekta ya umma ambayo ilichochea ukuaji wa sekta binafsi.

Alisema washiriki wa kongamano hilo watajadili na kuchangia maoni ya kisera na kimkakati ya kujenga sera na mifumo thabiti ya maendeleo ya uchumi wa jamii, huku wakiimarisha ulinzi wa kijamii kwa afya, kupitia ushirikiano wa kimkakati kati ya serikali.

"Tunajua kuwa, jukwaa la siku mbili halitoshi kufichua michango yote ya gwiji la Mheshimiwa Benjamin Mkapa inayohusu masuala haya ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi, lakini tunatumai mijadala yenye uthubutu itatuwezesha kwa ujasiri kufuata mtazamo wake wa kiutendaji, hisia ya mwelekeo," alisema.

Alisema serikali zote mbili ya Tanzania na Zanzibar zinatambua nafasi ya sekta binafsi katika kuharakisha maendeleo ya uchumi wa jamii na kufikia malengo ya maendeleo endelevu katika nchi.

Pia, alisema serikali zinatambua kwamba, ushiriki mkubwa wa sekta binafsi na wadau wasiokuwa wa kiserikali kupitia muungano wa biashara na sekta binafsi katika kutoa huduma bora, za kuaminika na zinazomudu, ni muhimu kwa ukuaji mpana na huduma za afya endelevu.

Alisema changamoto mbalimbali za mfumo wa afya kama vile upatikanaji mdogo wa huduma za afya kutokana na uwezo mdogo wa miundombinu, uhaba wa rasilimali watu kwa afya, upatikanaji mdogo wa teknolojia husika za afya, pamoja na nyingine nyingi, ni baadhi ya matatizo muhimu yanayokwamisha maendeleo ya kufikia huduma ya afya kwa wote.

Othman alimnukuu marehemu Mkapa kwa kusema: "Nimalizie kwa maneno ya Rais Mkapa kwenye hotuba yake kuu wakati wa mkutano wa SADC mwaka 2019, kwamba 'tunapaswa kupinga vishawishi vya kujenga kuta na sio madaraja'. Msemo huu una maana kwamba "uzio mzuri hufanya majirani wema."

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Benjamin Mkapa, Dk. Ellen Mkondya, alisema ni miaka miwili imepita bila ya kuwa na mwasisi wa taasisi hiyo, wanamkumbuka kwa mambo aliyokuwa akiyafanya wakati wa uhai wake.

Alisema kongamano hilo linalenga kujadili kumbukizi ya maisha ya Mkapa kwa yale aliyoyafanya wakati wa uhai wake.

Kwa upande wake Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema wanatambua mchango mkubwa unaotolewa na taasisi binafsi katika sekta ya afya na kwamba kongamano hilo liwe ni chachu katika kuongeza juhudi ya kusaidia jamii.

Alisema kupitia taasisi hiyo ambayo imeasisiwa na hayati Mkapa yapo maendeleo mengi yaliyofikiwa sio kwa sekta ya afya pekee bali hata kukuza uchumi wa taifa.

Hata hivyo, alisema kupitia taasisi hiyo kuna maboresho mengi yamefanyika katika sera za afya na katika ushirikiano wa sekta binafsi, alama zake sio rahisi kufutika katika Taifa la Tanzania.

Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, alisema serikali imenufaika kupitia Taasisi ya Mkapa kwa sababu imesaidia kuboresha huduma za afya na kuajiri wahudumu wa afya 37 kwa ajili ya kuhudumia jamii hasa katika maeneo ya vijijini kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wananchi Unguja na Pemba.

Alisema serikali itaendelea kutoa huduma bora kuanzia hospitali za wilaya na rufani kwa kuweka vifaa tiba dawa na kutoa mafunzo kwa watendaji wake.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA**
**MAHALI: KIGOMA**
**MAOMBI NA. 9192 MWAKA 2022**
**ANTONY MHOMOLI: MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MATHAYO WILSON: MJIBU MAOMBI**

## WITO/KUITWA SHAURINI

**KWA: MATHAYO WILSON POPOTE ULIPO**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kusikilizwa tarehe 19 Mwezi 07 Mwaka 2022 Saa 2.30 Asubuhi mbele ya Mheshimiwa M. MWINYI Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu mimi na Lakiri / Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 30 Mwezi wa 06, Mwaka 2022.

MWENYEKITI

..................................

**MWENYEKITI**

*The land Disputes Courts ( The District Land and Housing Tribunal) Regulations GN.No.*

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MOSHI DISTRICT REGISTRY**
**AT MOSHI**
**BILL OF COST NO.7 OF 2020**
**EDWARD HELGARD SAM ............DECREE HOLDER**
**VERSUS**
**PRIDE TANZANIA**
**GRM AUCTIONEER & COURT BROKER......JUDGEMENT DEBTOR ROBERT KIMARO**
**TO:**
**PRIDE TANZANIA , WHEREVER YOU ARE.**

**NOTICE FOR MENTATION,**

**TAKE NOTICE :** That the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at Moshi on 22nd September,2020 at 09:00 am before Honourable O.H. KINGWELE -Deputy Registrar.

**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Nipashe newspaper.

You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NORE THAT:** in default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this 14th day of August ,2020

O.H.KINGELE
DEPUTY REGISTRAR

**O.H.KINGELE**
**DEPUTY REGISTRAR**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No.90 of 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE EDWINI MRINDOKO MTUNDU**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY DOROTH JASTINIANI RWECHUNGURA**

## GENERAL CITATION
**(Rule 75 of Probate Rules)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the
**11 Day of AUGUST, 2022**
**Dated at Dodoma this 15th day of June,2022**

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......36/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: AKWILINA M.MATERU WA MAFISA-MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA...KURUTHUMU JUMA SEIF**

## TANGAZO

***(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 20 Mwezi 07 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 12 Mwezi 07 Mwaka 2022**

**HAKIMU**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 79 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late ELLY AIZACK MDINGI**

**By 1. JOYCE ELLY AIZACK**
**2. ......................................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 28 day of July..... 2022

Dated at MOROGORO this 13 day of July...2022

.....................................
**RESIDENT MAGISTRATE**


# OFISI ZA MATANGAZO
# MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
# PO.BOX 31042,
# DAR ES SALAAM.
# MOB: +255 - 0782253676

## KWA HABARI MOTOMOTO
## USIKOSE GAZETI
## LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Wagombea 8 wakabiliwa na kura ya mchujo

**LONDON,** Uingereza

WABUNGE wa chama cha Conservative huko Uingereza leo watapiga kura ya kuwachuja wagombea wanane wanaowania kuichukua nafasi ya Boris Johnson kama kiongozi wa chama hicho na waziri mkuu.

Haya yatafanyika wakati ambapo kambi hasimu katika chama hicho zinazozana katika kinyang'anyiro cha uongozi kilicholeta mgawanyiko.



Wagombea watatu kati ya 11 waliokuwepo awali walijiondoa jana baada ya kushindwa kupata uungwaji mkono wa kutosha ila idadi ya wanaowania nafasi hiyo bado ni kubwa.

Waziri wa zamani wa fedha Rishi Sunak ndiye anayepigiwa upatu kuichukua nafasi hiyo.

Nadhim Zahawi na Waziri wa Mambo ya Nje Liz Truss ni miongoni mwa wagombea wengine.

Wagombea wote watahitajika kupata angalau kura 30 kutoka kwa wabunge 358 wa chama hicho ili wafuzu kwenye raundi inayofuata ya upigaji kura.

## Biden aanza ziara Mashariki ya Kati

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani Joe Biden anatarajiwa kuanza ziara yake ya kwanza ya Mashariki ya Kati tangu achukue madaraka miezi 18 iliyopita atakapowasili mjini Jerusalem leo.

Atakapowasili huko Biden amepangiwa kufanya mazungumzo na Waziri Mkuu wa Israel Yair Lapid, Rais Isaac Herzog na kiongozi wa upinzani Benjamin Netanyahu.

Ikulu ya White House imesema atakapokuwa Israel, Biden atasisitiza dhamira ya Marekani ya usalama na ustawi wa Israel.

Amepangiwa pia kufanya mazungumzo na Rais wa mamlaka ya ndani ya Palestina Mahmoud Abbas katika Ukingo wa Magharibi, ambapo atasisitiza hatua yake ya kuunga mkono suluhu la mataifa mawili kwa kuwapa Wapalestina usalama sawa, uhuru na fursa.

Hapo kesho kutwa Ijumaa, rais huyo wa Marekani atasafiri kuelekea Saudi Arabia ambapo atakutana na viongozi wa nchi hiyo ya kifalme mjini Jeddah kisha ahudhurie mkutano wa kilele wa Baraza la Ushirikiano la Ghuba.

# Rais Sri Lanka aikimbia nchi, yatangazwa hali ya dharura

**COLOMBO,** Sri Lanka

SRI Lanka imetangaza hali ya dharura baada ya Rais Rajapaksa na mke wake kukimbilia nchini Maldives, saa chache kabla ya kufika kwa muda wake wa kuachia ngazi. Waziri Mkuu Ranil Wickremesinghe amekuwa kaimu rais.

Baada ya Rais Rajapaksa kukimbia, ofisi ya waziri mkuu ilitangaza hali ya dharura.

Licha ya kutangazwa hatua hiyo maelfu ya waandamanaji waliendelea kumiminika katika ofisi ya waziri mkuu Ranil Wickremesinghe, wakimtaka ajiuzulu.

Hata hivyo, polisi walijibu kwa kufyatua mabomu ya machozi.

Msemaji wa waziri mkuu, Dinouk Colombage alisema kiongozi huyo kama kaimu rais ametangaza hali ya dharura kote nchini humo na kuweka marufuku ya kutembea usiku katika mkoa wa magharibi.

Mapema jana, ofisa wa uhamiaji alisema rais na mke wake, pamoja na walinzi wawili, waliondoka nchini humo kwa ndege ya jeshi la Sri Lanka.

**Utorokaji huo unatokana na maandamano makubwa yanayoendelea katika taifa hilo, ambalo limekuwa likikabiliana na mzozo mbaya wa kiuchumi.**

Chanzo kutoka serikalini kilisema ndege hiyo ilitua katika mji mkuu wa Maldives, Male, na baadaye kuthibitishwa na jeshi la anga la Sri Lanka.

Utorokaji huo unatokana na maandamano makubwa yanayoendelea katika taifa hilo, ambalo limekuwa likikabiliana na mzozo mbaya wa kiuchumi.

Raia bado wanaendelea kushikilia makazi ya rais, huku wakitoa wito kwa waziri mkuu naye kujiuzulu.

### MAPAMBANO YANAENDELEA

Maandamano hayo ya umma yalimlazimisha Rajapaksa kwenda mafichoni na kukubali kuachia madaraka jana.

Hata hivyo Rajapaksa anakabiliwa na mashtaka kadhaa ya uhalifu na inaaminika aliondoka nchini humo kabla ya kujiuzulu na kupoteza kinga yake ya urais.

Hata hivyo mwanaharakati Chintaka Pradeep, alisema kukimbia hakutomsaidia Rajapaksa.

"Hakukuwa na njia kwa rais kusalia nchini. Amekuwa mafichoni wakati wote huu hivyo atalazimika kuishi nje ya nchi." Alisema.

Kabla ya kukimbia, Rais Rajapaksa alimteuwa waziri mkuu kuwa kaimu rais kulingana na muongozo wa katiba. Waziri mkuu Wickremesinghe pia atajiuzulu endapo muafaka utafikiwa juu ya kuundwa kwa serikali ya umoja.

Upo uwezekano kwamba Spika wa Bunge, Mahinda Yapa Abeywardena, atachukuwa uongozi wa nchi hadi rais mpya atakapochaguliwa, katika kura itakayofanyika Julai 20.

Kiongozi wa chama kikuu cha upinzani, Sajith Premadasa, aliyeshindwa na Rajapaksa katika uchaguzi wa rais wa mwaka 2019, alisema atawania nafasi hiyo.

Baadhi ya wanachama wa chama tawala wametoa wazo la Wickremesinghe kuwania nafasi ya rais.

Lakini wanaharakati wameapa hawatomtambua kama rais hata akigombea.



Waziri Mkuu wa Sri Lanka ambaye ni kaimu Rais wa sasa wa nchi hiyo akiwa katika Ikulu ya nchi hiyo alipokuwa akiapishwa kama Waziri Mkuu. **PICHA: MTANDAO**

# Ukraine yalishambulia ghala la Russia

**KYIV,** Ukraine

JESHI la Ukraine limesema limefanya mashambulizi ya maroketi ya masafa marefu kusini mwa Ukraine na kuharibu ghala la silaha za Russia.

Hata hivyo, vikosi vya Russia vinaendelea kufanya mashambulizi yake mashariki mwa Ukraine.

Taarifa ya jeshi hilo ilisema shambulizi hilo katika ghala hilo la Nova Kakhova mjini Kherson limewauwa watu 52. Shirika la habari la Russia, la TASS limeripoti kuwa utawala wa eneo hilo uliowekwa na nchi hiyo umesema karibu watu saba wameuwawa na takriban 70 kujeruhiwa. Shambulizi hilo limefanyika wakati ambapo Marekani imeitumia Ukraine silaha za kisasa aina ya HIMARS ambazo Ukraine inasema wanajeshi wake wanazitumia ipasavyo.

Wakati huo huo wizara ya ulinzi ya Russia imesema majeshi ya nchi hiyo yamezidungua ndege tatu za kivita za Ukraine mashariki mwa nchi hiyo.

Shirika la habari la Reuters limesema halikuweza kuthibitisha hayo yaliyotokea katika uwanja wa mapambano.

### UTURUKI, RUSSIA, UKRAINE KUFANYA MAZUNGUMZO

Ujumbe wa kijeshi wa Russia, Ukraine na Uturuki unatarajiwa kukutana na maofisa wa Umoja wa Mataifa mjini Istanbul jana kwa ajili ya mazungumzo ya uwezekano wa kupatikana kwa maelewano ya kuanza tena usafirishaji wa nafaka za Ukraine kutoka bandari kuu iliyoko katika Bahari Nyeusi ya Odesa.

Haya yanafanyika wakati ambapo mzozo wa chakula duniani unazidi kuwa mbaya zaidi. Wanadiplomasia walisema miongoni mwa yatakayokuwa kwenye mpango huo utakaojadiliwa ni vyombo vya kijeshi vya Ukraine kuzisindikiza meli za nafaka zinazotoka na kuingia katika bandari ya Odesa.

Pia Russia inatakiwa kukubali kusitisha mapigano wakati meli hizo zinapofanya safari zake kwenda Uturuki na Umoja wa Mataifa utafanya ukaguzi wa meli hizo. **DW**

# MAJALIWA MGENI RASMI MBIO ZA KOROSHO 2022

**Na Shufaa Lyimo**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mbio za Korosho Marathon zinazotarajiwa kufanyika Julai 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nagwanda Sijaona ulioko mkoani Mtwara, imefahamika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mratibu wa mbio hizo, Kajiru Kajiru alisema maandalizi kuelekea mashindano yanaendelea vizuri na wanawaomba wanariadha kutoka shemu mbalimbali kujiandikisha kushiriki.

Kajiru alisema kutakuwa na mbio za umbali wa kilomita 21, kilomita 10 na kilomita tano.

Mratibu huyo alisema asilimia 45 ya fedha ambazo zitapatikana katika mbio hizo zitapelekwa kwa wabanguaji wadogo wadogo wa korosho ambao hawana mashine ili kuwasaidia kuandaa korosho zao kisasa.

"Tunafahamu walimaji wengi wanabangua korosho kwa kutumia mikono, sasa fedha hizi zitawasaidia kuziandaa korosho zao kisasa," alisema Kajiru.

Aliongeza katika mbio jizo kutakuwa na zawadi mbalimbali za fedha pamoja na medali kwa washindi.

"Mshindi wa kwanza wa kilomita 21 atapata kiasi cha Sh. milioni tano, mshindi wa pili Sh. milioni nne, mshindi wa tatu Sh. milioni tatu, mshindi wa nne milioni mbili, mshindi wa tano milioni moja huku atakayeshika nafasi ya sita ataondoka na kiasi cha Sh. 500,000," Kajiru alisema.

Aliongeza kwa upande wa mbio za kilomita 10 mshindi wa kwanza atapata Sh. milioni mbili, mshindi wa pili atajinyakulia Sh. milioni moja na mshindi wa tatu atakabidhiwa Sh. 500,000 huku mbio za kilomita tano mshindi wa kwanza atapata Sh. 500,000 huku mshindi wa pili atapata Sh. 300,000 na mshindi wa tatu atapata Sh. 100,000.

"Zawadi zitatolewa kwa washindi wote ambao watakuwa wamefanya vizuri katika mashindano hayo, lengo ni kuwakutanisha pamoja watanzania kupitia mbio hizo," alisema Kajiru.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho, Ahadiel Mmbughu, alisema mashindano hayo yatashirikisha watu wa jinsia zote bila kujali umri.

Mmbunghu alisema lengo la mbio hizo ni kuwafahamisha Watanzania watambue jinsi ya kutumia bidhaa zitokanazo na zao la Korosho ikiwamo kuona fursa mbalimbali zitokanazo na zao hilo.



Mchezaji wa timu ya soka ya vijana ya umri chini ya miaka 17 ya Pan Africans (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya nyota wa Yanga katika mechi ya Ligi ya U-17 iliyochezwa kwenye Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam jana asubuhi. Yosso wa Yanga walishinda mabao 3-0. **PICHA : TFF**

# JKT Mbweni kinara netiboli

**Na Adam Fungamwango**

JKT Mbweni iko kileleni katika Ligi ya Netiboli Daraja la Kwanza baada ya kuichapa Chuo Kikuu cha Kampala mabao 56-23 katika mchezo uliochezwa mapema wiki hii kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Kwa matokeo hayo, JKT Mbweni imefikisha pointi sita baada ya kupata ushindi wa mabao 55-43 katika mechi yake ya kwanza dhidi ya Magereza Morogoro halafu ikaigalagaza Eagle Queens mabao 57-20.

Nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo inashikiliwa na Nyika ambayo pia ina pointi sita lakini imezidiwa mabao 10 na JKT Mbweni, baada ya kushinda mechi tatu, ikiifunga UDSM mabao 42-19, ikaifyatua Eagle mabao 63-22, kabla ya kuiangamiza Polisi Arusha mabao 53-29.

JKT Mbweni imefunga mabao 168, huku Nyika ikiwa na ikiwa na mabao 158.

Katibu Mkuu wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), Rose Mkisi alisema ligi hiyo iliyoanza tangu Julai 9 mwaka huu, huku mechi mbalimbali zikipigwa asubuhi na jioni.

Alizitaja timu zinazoshiriki ligi hiyo ni pamoja na JKT Mbweni, Nyika, TAMISEMI Dodoma, Magereza Moro, Polisi Moro, Polisi Arusha, Eagle Queens, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Kampala kilichopo Dar es Salaam.

## Morocco kuinoa KMKM kimataifa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

UONGOZI wa KMKM umeingia makubaliano na Kocha, Hemed Suleiman 'Morocco' kwa ajili ya kukinoa kikosi chake katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

KMKM ndio mabingwa wa Ligi Kuu Zanzibar na ndio watakaopeperusha bendera ya visiwa hivyo katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa KMKM, Sheha Mohamed alisema makubaliano hayo kwa hatua ya awali ya mashindano ya CAF pamoja na mzunguko wa kwanza wa msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar 2022/2023.

Sheha alisema licha ya kumpa muda mfupi kukinoa kikosi hicho lakini timu hiyo baadaye inaweza kumpatia mkataba wa kudumu wa kukiongoza kikosi hicho kulingana na mafanikio yake.

"Tumempa mkataba mfupi kwa ajili ya kutuongoza katika hatua ya awali ambapo malengo yetu makubwa ni kufanya vizuri kwenye michuano ya kimataifa, lakini pia kuendelea naye katika msimu huu," alisema Sheha. Alisema uamuzi wa kumchukua kocha huyo ni kwa sababu ana uzoefu na mashindano ya kimataifa huku akiongeza kikosi chao kitaanza mazoezi kesho.

## Shusho ashushia nondo wanawake

**Na Sabato Kasika**

MWIMBAJI wa nyimbo za Injili, Christina Shusho, amewataka wanawake wenzake waachane na dhana potofu ya kuamini wanaume wote ni wakorofi, bali watambue wapo wengi ambao ni wema.

Shusho alisema katika video yake aliyorusha katika mitandao ya kijamii, huku akikiri ni kweli wapo wanaume wakorofi na wenye kila aina ya tabia mbaya, lakini si wote wa aina hiyo.

"Tusaidiane kuondoa dhana hii, 'wanaume wote wako hivyo', wapo wakali, lakini pia wapo wapole, wapo wahuni lakini pia wapo wema na waungwana, wapo wasio na elimu na wapo wasomi," alisema Shusho.

Alisema, katika mazingira hayo, ni makosa kukumbatia dhana kwamba wanaume wote hawafai, ambapo amewataka wenzake kutokata tamaa wanapotafuta wachumba, badala yake wahakikishe wanatafuta kwa umakini.

Mwimbaji huyo alisema, anajua kuna elimu nyingi ambazo wanawake wanakutana nazo zikiwamo zinazowakwamisha kupata wachumba kwa kuamini dhana hiyo ikiwamo ya kwamba wanaume wote si waaminifu.

## ZISIKUPITE

### RAPHINHA KUTUA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Leeds United na Timu ya Taifa ya Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 25, anatarajiwa kusafiri kuelekea Barcelona kukamilisha uhamisho wake wa kutua Nou Camp. ***(Athletic)***

### LEEDS KUPATA NEEMA

LEEDS United imekubali ofa ya pauni milioni 49 ambayo itapanda na kufikia pauni milioni 57 kutoka kwa Barcelona ili kumwachia Raphinha. ***(Guardian)***

### ISAK MAMBO SAFI

NEWCASTLE United imefanya mazungumzo na Real Sociedad kuhusu kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 22 kutoka klabu hiyo ya Hispania kwa uhamisho utakaoweka rekodi ya klabu. ***(Telegraph)***

### KIMPEMBE KUTUA CHELSEA

CHELSEA imeonyesha nia ya kumnasa mlinzi wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Presnel Kimpembe mwenye umri wa miaka 26. ***(Telegraph)***

### RONALDO AMTAKA MESSI

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, anataka kutua Paris St-Germain kujaribu kucheza pamoja na Lionel Messi (35), baada ya kusema anataka kuondoka Manchester United. ***(Le Parisien, via Express)***

### TOMAS ATAJWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inamtaka mshambuliaji wa Espanyol na Timu ya Taifa ya Hispania, Raul de Tomas mwenye umri wa miaka 27. ***(Ekrem Konur)***

### RICE KUBAKI WEST

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya England, Declan Rice amekubaliana na West Ham kusalia klabuni hapo angalau kwa msimu mmoja zaidi kabla ya nyota huyo mwenye miaka 23 kuruhusiwa kutimka. ***(Talksport)***

### CHELSEA, BARCA VITANI

CHELSEA imepeleka ofa ya kujaribu kuizidi kete Barcelona ya kumnasa mshambuliaji mkongwe wa Timu ya Taifa ya Poland, Robert Lewandowski anayetaka kuondoka Bayern Munich na kutua Barcelona. ***(Mirror)***

### MARTINEZ AKARIBIA UNITED

MANCHESTER United iko mbele ya Arsenal katika mbio za kumwania mlinzi wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lisandro Martinez mwenye umri wa miaka 24 kutoka Ajax. ***(Goal)***

### JORGINHO: NAIPENDA CHELSEA

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 30, ambaye amebakisha mwaka mmoja katika mkataba wake na Chelsea, amesema angependa "kusalia" kwenye klabu hiyo ya Stamford Bridge licha ya kuhusishwa kutimmka. ***(Athletic)***

### AZPILICUETA BADO YUPO

MLINZI wa kulia wa Timu ya Taifa ya Hispania, Cesar Azpilicueta anataka kutua Barcelona, lakini Chelsea imemfahamisha beki huyo mwenye miaka 32 kwamba, watamruhusu kuondoka iwapo watafanikiwa kusajili mlinzi mwingine. ***(Mail)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG : UNITED BADO HAIJAIMARIKA

Kocha huyo asema bado ana kazi kubwa ya kukiimarisha kikosi chake...

**BANGKOK, Thailand**

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amesema licha ya timu yake kuifunga Liverpool mabao 4-0 katika mechi yake ya kwanza kuinoa, bado kuna kazi kubwa ya kufanya ingawa aliridhika na mwanzo mzuri.

Mabao ya kipindi cha kwanza kutoka kwa Jadon Sancho, Fred, Anthony Martial yalimfanya kocha huyo wa Uholanzi kuwa na mwanzo mzuri katika mechi yao ya kirafiki ya kujiandaa na msimu mpya mjini Bangkok kabla ya Facundo Pellistri kuongeza bao la nne baadaye na kukamilisha ushindi mnono.

United ilichukua fursa ya Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp, kutaja timu dhaifu kwa pambano hilo, huku mastaa kama Mohamed Salah, Virgil van Dijk na Darwin Nunez wakiingizwa kuanzia dakika ya 61.

Na ingawa kulikuwa na kiwango chanya kwa United walipokuwa wakiwaweka wapinzani kwenye wakati mgumu, Ten Hag anajua bado ni mapema mno kukubali kikosi chake ni kizuri.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 52 aliiambia MUTV: "Najua tuna wachezaji wazuri, sasa tunapaswa kuunda timu. Nina furaha na mchezo wa kwanza.

"Itachukua muda mwingi kuiwezesha timu hii kucheza kwa namna yangu, nimeona makosa mengi leo (juzi), tuseme ukweli, Liverpool walichezesha timu tatu, hawakuwa kwenye nguvu zao.

"Hatupaswi kukadiria matokeo haya, lakini bado nimeona mambo mazuri. Tuna ubunifu mwingi na kasi mbele. Kama nilivyosema, tuna uwezo.

"Nadhani hiyo ilikuwa timu yenye ari kubwa na tunajua ndiyo kwanza tumeanza. Tulifanya makosa, lakini pia tulitengeneza nafasi kadhaa nzuri na tukapata mabao."

Ushindi huo kwenye Uwanja wa Rajamangala pia ulimfanya mchezaji aliyesajiliwa kwa pauni milioni 13, Tyrell Malacia, kucheza mechi yake ya kwanza, kwani beki huyo wa kushoto alichukua nafasi ya Luke Shaw kipindi cha pili.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI

FC RIGA
VERSUS
DERRY CITY

1 | 1.75
X | 3.47
2 | 4.73

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CHELSEA NJIA NYEUPE KUMNASA KOULIBALY



**LONDON,** England


CHELSEA wana matumaini ya kukamilisha mpango wa kumsajili beki wa kati, Kalidou Koulibaly, huku mchezaji huyo akitaka kuhamia London, Napoli hawataki kufanya biashara na wapinzani wao wa Serie A, Juventus, kwa mujibu wa 90min.

Akiwa amejiunga na Napoli mwaka wa 2014, Koulibaly ameingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake na sasa anahitaji kupata changamoto mpya katika maisha yake.

Chelsea wako sokoni kutafuta mabeki wa kati msimu huu wa joto baada ya kuwapoteza, Antonio Rudiger na Andreas Christensen kama wachezaji huru kwa Real Madrid na Barcelona, na wanaweza kusajili hata nyota watatu ikiwa kocha, Thomas Tuchel atakubali.

Kwa mujibu wa 90min, Kouliably amekuwa akichukuliwa kuwa chaguo namba moja, huku Chelsea ikiwasiliana na wawakilishi wake mapema msimu huu wa joto, na mazungumzo ya kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 sasa yanazidi kushika kasi.

Maslahi binafsi hayatakuwa suala kwa klabu hiyo, na Koulibaly ameonyesha nia ya kuelekea London Magharibi.



## De Ligt akaribia Bayern Munich

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich wanazidi kujiamini kukamilisha dili la kumsajili, Matthijs de Ligt kutoka Juventus, kwa mujibu wa 90min.

Mholanzi huyo amekuwa akihusishwa kwa kiasi kikubwa na Chelsea na Bayern Munich katika miezi ya hivi karibuni, lakini kufuatia mazungumzo chanya mjini Turin kati ya Hasan Salihamidzic na wakurugenzi wa Juventus siku ya Jumatatu, Bavaria hao sasa wanaonekana huenda wakamtwaa De Ligt.

Wakati wa kuondoka kwenye mazungumzo siku ya Jumatatu, Mkurugenzi wa Bayern Munich, Salihamidzic, alipoulizwa kuhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, alisema: "Tutaona, siwezi kusema chochote kuhusu mkataba wa Matthijs de Ligt. Matumaini? Daima tuna matumaini".

Matumaini kuhusu makubaliano yanawezekana, na 90min iliripoti wiki iliyopita kwamba, wakati Chelsea walikuwa wakivutiwa, Bayern Munich waliamini kwa sasa ndio wenye nafasi zaidi kumtwaa De Ligt, huku beki huyo akifurahishwa na mradi uliopendekezwa kwa wawakilishi wake na mkurugenzi wa michezo Salihamidzic na Kocha Mkuu, Julian Nagelsmann.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# MATATANI AKIUZA JEZI FEKI ZA SIMBA, YANGA

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linamshikilia mfanyabiashara, Said Furaha kwa kosa la kuuza jumla ya jezi bandia dazani 145 zenye nembo ya Simba na dazani 151 ya Yanga.

**Jezi za Simba rasmi zimeruhusiwa kuuzwa na mfanyabiashara anayejulikana kwa jina la Vunja Bei na zile za Yanga zinatakiwa kuuzwa na Kampuni ya GSM.**

Nguo hizo zilikamatwa Julai 5, mwaka huu na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na maofisa masoko kutoka GSM na Vunja Bei katika maeneo ya barabara ya Pamba sokoni wilayani Nyamagana jijini hapo.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhan Ng'anzi alisema jana wanamshikilia Furaha (31) kwa ajili ya upelelezi.

"Baada ya kupata taarifa kutoka kwa maofisa masoko wa kampuni ya GSM na Vunja Bei kuwa kuna mfanyabiashara anasambaza na kuuza jezi bandia tukafanya uchunguzi ndipo tukambaini, Said Furaha ambaye alikuwa na jumla ya jezi bandia za Simba na Yanga dazani 296 kinyume na sheria," alisema Ng'anzi.

"Mtuhumiwa huyo tunamshikilia na upelelezi unaendelea kuhusiana na shauri hili ili kubaini mtandao mzima wa wahusika wote wanaotengeneza, kuagiza na kuingiza nchini bidhaa hizi bandia na mtuhumiwa atafikishwa mahakamani haraka iwezekanavyo," aliongeza.

Kwa upande wao maofisa wa masoko wa kampuni ya GSM na Vunja Bei waliwataka mashabiki wa timu hizo kuepuka kununua jezi bandia ili kuepusha hasara kwa timu zao.

"Ununuaji wa vitu bandia vya timu unagharimu timu nzima kwa ujumla ikiwamo wakurugenzi na wadhamini wa timu hiyo kwani hasara hii inazifanya timu zetu kushindwa kujihudumia niwaombe kutoa taarifa kwa yeyote anayejihusisha na ununuzi wa jezi hizo," alisema Maksen Omary, Msimamizi GSM tawi la Mwanza.

"Tunalishukuru Jeshi la Polisi mkoani Mwanza kwa ushirikiano wao katika kudhibiti vitendo vya usambazaji na uuzaji wa jezi bandia za timu yetu, niwaombe wapenzi wa hii timu kutoa ushirikiano pindi mnapogundua kuna udanganyifu katika usambazaji wa jezi zetu," alisema Said Markela ambaye ni Meneja wa Vunja Bei, Mwanza.




Balozi wa China, Chen Mingjian (katikati), akimkabidhi kompyuta Katibu Mtendaji wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Neema Msitha kwa ajili ya matumizi ya ofisi ya Kamati ya Paralimpiki Nchini (TPC). Kamati hiyo imepokea vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 20. **PICHA: SHUFAA LYIMO**

# *Sopu: Sitaisahau Coastal Union*



**Na Adam Fungamwango**

MSHAMBULIAJI Abdul Suleiman 'Sopu' amesema licha ya kujiunga na Azam FC, kamwe hataisahau Coastal Union kwa sababu ndiyo iliyomtangaza na kumweka sokoni, hivyo inaendelea kuwa moyoni mwake daima.

Wakati Sopu akisema hiyo, kiungo Victor Akpan, aliyetambulishwa na Simba naye aliishukuru klabu hiyo pamoja na viongozi wake kwa kusema yeye ni kama mtoto anayetoka nyumbani kwao kwenda kutafuta maisha mbali na hapo.

Wachezaji hao walisema hayo kwenye hafla na mchezo maalum ya kuwaaga uliochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga.

"Naweza kusema Coastal ndiyo timu yangu, naondoka lakini nitaikumbuka sana. Imenitangaza na kujulikana, imenionyesha mbele za mashabiki mimi ni nani, kusema kweli iko moyoni mwangu daima," alisema Sopu.

Kocha Mkuu, Juma Mgunda aliwashukuru wachezaji hao na kuwatakia kila la kheri kwenye maisha mapya ya kisoka.

Mwenyekiti wa Coastal Union, Steven Mguto aliwatakia kheri, lakini akawataka wasiisahau klabu hiyo kwa sababu ndiyo iliyowapa hatua moja kwenda mbele.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU,
BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## ALHAMISI - 14/07/2022


| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4670 | Dhaka Abahani vs Shadhinata Krira Sangha | 1.38 | 4.80 | 6.80 |
| 14:00 | 3017 | Stabaek Fotball 2 vs Os TF | 4.02 | 4.42 | 1.60 |
| 16:00 | 2431 | Racing Club Reserve vs Newells Old Boys | 2.34 | 3.10 | 2.86 |
| 16:00 | 3055 | Argentinos Juniors Reserve vs CA Barracas Central Reserve | 1.41 | 4.24 | 6.50 |
| 17:00 | 1564 | Atletico Tucuman Reserve vs CA Aldosivi Reserve | 2.31 | 3.30 | 2.90 |
| 17:00 | 1819 | Rosario Central Reserve vs Independiente Reserve | 2.02 | 3.28 | 3.33 |
| 17:00 | 4228 | FK Liepaja vs KF Gjilani | 1.54 | 3.89 | 6.06 |
| 18:00 | 1782 | Akademija Pandev vs Lechia Gdansk | 6.45 | 4.43 | 1.45 |
| 18:00 | 4956 | College Europa vs Vikingur Gota | 2.43 | 3.43 | 2.72 |
| 18:00 | 5767 | Ararat Yerevan vs Shkendija | 2.61 | 3.37 | 2.56 |
| 19:00 | 1507 | Zalgiris Kaunas vs Ruzomberok | 3.63 | 3.43 | 1.99 |
| 19:00 | 2114 | Paide Linnameeskond vs Dinamo Tbilisi | 4.35 | 4.04 | 1.69 |
| 19:00 | 2121 | FK Sloga Simin Han vs Tre Penne Galazzano | 1.05 | 11.02 | 35.06 |
| 19:00 | 2797 | Seinajoen JK vs Flora Tallinn | 2.83 | 3.28 | 2.43 |
| 19:00 | 3238 | Italy W vs Iceland W | 2.05 | 3.34 | 3.19 |
| 19:00 | 5036 | Milsami Orhei vs FK Panevezys | 2.92 | 3.18 | 2.42 |
| 19:30 | 5109 | Eastern Company SC vs Misr Lel Makasa | 2.26 | 3.02 | 3.32 |
| 20:00 | 2001 | FC Riga vs Derry City | 1.75 | 3.47 | 4.73 |
| 20:00 | 2330 | Sandnes Ulf 2 vs Sola | 1.70 | 4.71 | 3.34 |
| 20:00 | 2965 | B36 Torshavn vs Borac Banja Luka | 4.45 | 3.74 | 1.73 |
| 20:00 | 3784 | Petrocub vs Floriana | 1.71 | 3.45 | 5.07 |
| 20:00 | 3829 | Cameroon W vs Nigeria W | 3.25 | 3.00 | 2.18 |
| 20:00 | 3859 | Dila Gori vs KuPS Kuopio | 2.43 | 3.34 | 2.78 |
| 20:00 | 4268 | Buchbach vs Unterhaching | 3.74 | 3.83 | 1.75 |
| 20:00 | 4416 | Atletic Club Escaldes vs Gzira United | 2.48 | 3.13 | 2.88 |
| 20:15 | 4565 | Newtown AFC vs HB Torshavn | 3.08 | 3.33 | 2.25 |
| 20:30 | 2545 | Differdange vs Olimpija Ljubljana | 3.59 | 3.39 | 2.01 |
| 20:30 | 4623 | Montana vs Etar | 2.50 | 3.04 | 2.70 |
| 20:30 | 4631 | Grei vs Lokomotiv Oslo FK | 2.84 | 3.92 | 2.03 |
| 21:00 | 1089 | NK Mura vs Sfintul Gheorghe | 1.27 | 5.44 | 10.08 |
| 21:00 | 1143 | Partizani Tirana vs Saburtalo Tbilisi | 2.23 | 3.27 | 3.17 |
| 21:00 | 1845 | KF Llapi vs Buducnost | 2.88 | 3.33 | 2.37 |
| 21:00 | 3756 | Sligo Rovers vs Bala Town | 1.46 | 4.45 | 6.28 |
| 21:00 | 4687 | Hamrun Spartans vs Alashkert Martuni | 2.44 | 3.08 | 2.98 |
| 21:15 | 2036 | KR Reykjavik vs Pogon Szczecin | 4.64 | 4.13 | 1.63 |
| 21:45 | 1399 | SP Tre Fiori vs Fola | 5.03 | 4.13 | 1.59 |
| 21:45 | 4701 | Decic Tuzi vs Dinamo Minsk | 3.38 | 3.33 | 2.11 |
| 21:45 | 5009 | Larne vs ST Josephs FC | 1.40 | 4.46 | 7.70 |
| 22:00 | 1243 | Cliftonville Belfast vs Dunajska Streda | 3.33 | 3.38 | 2.11 |
| 22:00 | 2456 | France W vs Belgium W | 1.12 | 6.89 | 15.75 |
| 22:00 | 4403 | Crusaders Belfast vs FCB Magpies | 1.49 | 4.34 | 5.86 |
| 22:00 | 5083 | Ceramica Cleopatra vs El Ittihad Alexandria | 2.11 | 3.06 | 3.66 |
| 22:00 | 5466 | Iskra vs Laci | 3.14 | 3.19 | 2.29 |
| 22:15 | 1009 | Fylkir vs Kordrengir | 1.85 | 3.73 | 3.44 |
| 22:15 | 2883 | Grotta vs UMF Selfoss | 1.74 | 4.21 | 3.47 |
| 22:15 | 3349 | Throttur Vogum vs UMF Grindavik | 4.43 | 4.33 | 1.55 |
| 22:15 | 3936 | Breidablik vs UE Santa Coloma | 1.14 | 7.07 | 19.18 |
| 22:15 | 4288 | HK Kopavogs vs KV Vesturbaer | 1.35 | 5.10 | 6.08 |
| 23:00 | 4740 | Sporting Lisbon vs Villarreal | 2.50 | 3.40 | 2.55 |
| 23:30 | 2810 | Puerto Quito vs Chacaritas FC | 2.60 | 2.85 | 2.75 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Alhamisi Julai 14, 2022

Nipashe



Ten Hag: United haijaimarika UKURASA 21



Winga wa Timu ya Soka ya Taifa ya Ghana, Augustine Okrah, ametambulishwa rasmi kuwa nyota mpya wa Simba. Okrah amejiunga na Wekundu wa Msimbazi akitokea, Bechem United ya Ghana. **PICHA: SIMBA SC**

## Geita Gold yapania CAF

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Geita Gold FC umeweka wazi wamejipanga kuboresha kikosi chao ili kuendeleza kasi walioionyesha msimu uliopita kwa kufanya vyema katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/2023 na mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika watakayoshiriki.

Geita Gold FC iliyomaliza katika nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika pamoja na Azam FC iliyoshika nafasi ya tatu itaziwakilisha nchi kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Geita, Zahara Michuzi, aliliambia gazeti hili jana anaamini watakuja kwa mwendo wa kipekee katika msimu ujao baada ya kupata uzoefu wa kukabiliana na changamoto mbalimbali kupitia msimu uliomalizika.

"Tumedhamiria msimu ujao kuwa bora na imara, tunaimarisha kikosi ili kiwe cha moto kwa kuotea mbali hasa wachezaji tunaowasajili wanakiwango kizuri na kupambania timu kufanya vizuri katika mashindano yaliyoko mbele yao," alisema Zahara.

Bosi huyo alisema wamejipanga kusuka kikosi chao kama ilivyopendekezwa na Kocha Mkuu, Felix Minziro kwa ajili ya kwenda kushindana katika michuano hiyo ya CAF.

"Pia tunaendelea kuimarisha miundombinu ikiwamo kumalizia ujenzi wa uwanja kwa ajili ya kuutumia kwenye mechi za ligi ya ndani," Zahara alisema.

# Simba, Yanga zakabana koo

**Na Saada Akida**

## Mnyama amtambulisha Okrah huku ujio wa staa Aziz Ki ukiendelea...

WAKATI Simba imemtambulisha rasmi kiungo mshambuliaji mpya, Augustine Okrah kutoka Bechem United kwa kumpa mkataba wa miaka miwili, mashabiki wa Yanga wameendelea kusubiri ujio wa nyota wao, Aziz Ki Stephano.

**Okrah ambaye ni raia wa Ghana ana uwezo pia wa kucheza nafasi ya winga na nyuma ya washambuliaji.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema klabu hiyo inatambulisha wachezaji mchana kwa sababu wachezaji wao wamewanunua na kuwatoa katika kikosi cha kwanza.

"Tunaendelea kutambulisha ila hatusajili wachezaji ambao hawako katika timu ya taifa wala si wale ambao walikaa benchi, wasiokuwapo katika kikosi cha timu za taifa," alisema na aliongeza;

"Usajili tuliofanya ni kusajili wachezaji ambao bado wana mkataba na klabu tuliyomchukua kwa kufanya biashara ndio maana tunatambulisha mchana kama ilivyo kwa Okrah," Ahmed.

Kiongozi huyo aliongeza Simba imeandaa mambo mazuri kwa ajili ya msimu ujao na maandalizi ya safari ya kuelekea Ismailia, Misri kuweka kambi yamekamilika.

"Simba inatarajiwa kusafiri kesho (leo) kuelekea Misri kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa, tukiwa huko tumejipanga kufanya mazoezi yatakayoimarisha timu yetu na kurudi na kasi," Ahmed alisema.

Aliongeza Simba imefanya usajili wake kwa malengo na matakwa ya benchi la ufundi na si kwa sababu ya mihemuko ya wanachama, mashabiki au kushindana na timu nyingine.

"Huu ni muda wa Simba sasa, baada ya utambulisho wa mchezaji wetu wa leo (jana) ambao tutaufanya tukiwa katika ardhi ya nyumbani ila waliobakia tutawatambulisha timu ikiwa Misri," alisema Ahmed.

Alieleza wanafahamu ushindani katika Ligi Kuu Tanzania Bara utaongezeka lakini wanahitaji kufanya vizuri na kufikia malengo kwenye michuano ya kimataifa chini ya kocha mpya Mserbia, Zoran Manojlovic.

"Kuhusu suala la makocha wa makipa na viungo hilo liko katika mchakato na timu itakapokuwa Misri kila kitu kitakuwa vizuri, kupatikana kwa walimu hao kutaliongezea nguvu benchi la ufundi," alisema kiongozi huyo.

Kiungo huyo msimu uliopita akiwa na Bechem United alicheza mechi 31 akifunga mabao 14 na kutengeneza nafasi za kufunga magoli nane.

Okrah kwa nyakati tofauti amewahi kuzitumikia timu za Asante Kotoko ya Ghana, Al Marreikh, Al Hilal (zote za Sudan), Smouha FC (Misri) na North East United (India).

Msemaji wa Yanga, Haji Manara ameendelea kusisitiza Aziz Ki ni mali yao na muda rafiki ukifika atawasili nchini kwa ajili ya utambulisho wa 'kibabe'.

"Ule wakati wa kutangaza usajili wa mchezaji mkubwa anayekuja klabu kubwa Afrika Mashariki na Kati unakaribia, tunaomba kama wewe sio Mwananchi, basi ni vyema ukatafuta mchezo mwingine wa kushabikia kabla ya msimu kuanza," alitamba Manara.

Alisema pia wanafuraha kuona beki wao, Abdallah Shaibu 'Ninja' amesaini mkataba mpya wa mwaka mmoja wa kuendelea kubakia klabuni hapo.

Dirisha la usajili litafungwa rasmi ifikapo Agosti 31, mwaka huu, wakati pazia la Ligi Kuu Tanzania Bara litafunguliwa Agosti 17, mwaka huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >